**Mwenyekiti** matatani kushawishi wananchi kususia ujenzi wa shule

UK. 3



**Serikali**, UNESCO kuimarisha uchumi vyombo vya Habari

UKURASA 4




UKURASA 9


# Nipashe Jumapili

Jumapili Juni 4, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0581331

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




## RIPOTI CAG ZANZIBAR:

# Haponi mtu

• **Waliotajwa** kuhusika madudu kwenda na maji, Dk. Mwinyi asema... *Ukurasa 2*



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan (katikati), akikata utepe kuzindua ndege mpya ya mizigo aina ya Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) hafla iliyofanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

## Historia yaandikwa ndege mizigo kutua nchini

UKURASA 3

## Mtaalamu ataja chanzo wanaume wengi kujiua

UK 2

MICHEZO **AZAM: FA MALI YETU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Hussein Ali Mwinyi, akizungumza katika viwanja vya Ikulu Jijini Zanzibar, wakati wa hafla ya kuwasilishwa kwa Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, iliyowasilishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar Dk. Othman Abbas Ali. **PICHA: IKULU**

# Haponi mtu madudu ripoti CAG Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HAPONI mtu. Ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuweka bayana kwamba serikali itachukua hatua mbalimbali zikiwemo za kiutawala na kijinai kwa mujibu wa sheria dhidi ya wahusika walitotajwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) Zanzibar.

Baada ya kupokea ripoti hiyo jana, Rais Mwinyi alisema waliothibitika kufanya ubadhirifu na uzembe ambao umesababishia serikali kupata hasara, utaratibu wa kuchukua hatua uko wazi. Ripoti hiyo ya CAG Zanzibar ya mwaka 2021/22 imeonyesha madudu yakiwamo upotevu wa fedha za umma na ubadhirifu uliokithiri katika miradi ya maendeleo.

Akiwasilisha ripoti hiyo jana, Ikulu, Zanzibar, CAG Dk. Othman Abbas Ali, alisema katika ukaguzi alioufanya, alibaini pia taasisi nane za serikali zilikuwa na hati chafu na zisizoridhisha.

Alizitaja taasisi hizo ni Wizara ya Fedha na Mipango, Hesabu Jumuishi za Mfuko Mkuu wa Serikali, Tume ya Ukimwi, Hospitali ya Mnazi Mmoja, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Maji, Nishati na Madini.

Dk. Othman alitaja mashirika ya umma na taasisi zinazojitegemea zilizobainika kuwa na hati zenye shaka na hati mbaya ni Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), Shirika la Bandari, Shirika la Bima na Wakala wa Usajili Matukio ya Kijamii.

Mengine ni Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mamlaka ya Usafiri Baharini, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar na Baraza la Manispaa ya Mjini.

Hivyo aliwataka maofisa fedha wa taasisi za umma kuongeza umakini katika usimamizi wa majukumu yao, kuongeza nidhamu katika usimamizi wa fedha na matumizi ya rasilimali za umma.

Pia aliwataka maofisa fedha kuwajengea uwezo watendaji wa taasisi zao ili kukabiliana na majukumu yao ya kazi kwa kuzingatia misingi ya sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa fedha za umma.

Aidha, alisema tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wake kwa mwaka wa fedha uliopita mapendekezo 2,820 aliyatoa kati ya hayo 1,237 yalifanyiwa kazi, 659 yanaendelea kutekezwa, 442 hayakutekelezwa, 340 yamejirudia na 142 yamepitwa na wakati.

### USIMAMIZI MAPATO

Dk. Othman alisema kukosekana kwa ufafanuzi wa taarifa ya bakaa ya fedha ambayo haikutumiwa na taasisi za umma na kuripotiwa na hesabu jumuishi ya serikali ya Sh. bilioni 415 kwa mwaka 2021/22 kwa wizara, idara na mikoa.

Alisema alibaini kuwa Sh. trilioni 1.546 zilionyesha katika hesabu jumuishi za serikali kuwa ni mapato halisi na Sh. bilioni 415 zilikosa ufafanuzi.

Mapato ambayo hayakuripotiwa katika ufungaji wa hesabu, alisema ni Sh.bilioni 9.69 na taasisi 10 ziliwasilisha taarifa za hesabu zao kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi bila ya kubainisha uwepo wa mapato yaliokusanywa kupitia vyanzo vyao vya mapato. Alisema hali hiyo ilisababisha serikali kushindwa kukamilisha mipango ya maendeleo. Dk. Othman alisema pia alibaini malipo yaliofanyika kwa makandarasi bila ya kuzingatia masharti ya mikataba ya Sh. bilioni 11.74.

Alisema pia ripoti imebainisha usimamizi wa bajeti ya mfuko wa usimaizi wa miundimbinu usioridhisha kwa sababu baadhi ya watekelezaji wa miradi kushindwa kumalizia kazi zao kutokana na miradi husika kupokea kiwango kidogo cha fedha kinyume na bajeti iliyopangwa.

### DAWA BANDIA

Alisema pia amebaini uwepo wa dawa na vifaa tiba vilivyopitwa na muda wa matumizi ambavyo ni hatari kwa matumizi ya binadamu. Dawa hizo na vifaa tiba, alisema vimekutwa katika Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar na katika vituo mbalimbali vya afya.

Alisema miongoni mwa vifaa tiba hivyo vilifanyiwa majiribio na kuleta majibu ya kwamba mwanaume aliepimwa alikutwa na ujauzito.

Pia lisema kuna matumizi mabaya ya fedha za uviko-19 katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo, afya, elimu, miundombinu ya maji na uchumi wa buluu na uvuvi.

### KAULI YA RAIS

Akizungumza baada ya kupokea ripoti hiyo, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema serikali bado ina kazi kubwa ya kufanya juu ya udhibiti wa mapato na matumizi ya serikali.

Alisema serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo za kiutawala na kijinai ili waliohusika wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za nchi. Pia alisema wote waliothibitika kufanya ubadhilifu na uzembe ambao umesababishia serikali kupata hasara utaratibu wa kuchukua hatua upo wazi.

Alisema ni lazima ZAECA kupitia kasoro zote hasa zile zinazoashiria wizi na ubadhilifu wa mali za umma na kuitaka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kufanya kazi kwa karibu na vyombo vyengine ili kuona wanaipa umuhimu ripoti hiyo ili kila mwaka mafanikio yawe mengi zaidi kuliko upungufu.

# Mtaalamu ataja chanzo wanaume wengi kujiua

**Na Mary Geofrey**

TATIZO la kurithi, ugonjwa wa akili na ugumu wa maisha vimetajwa kuwa visababishi vikuu vya wanaume wengi kuchukua uamuzi wa kujiua kuliko wanawake.

Katika siku za hivi karibuni kumekuwa na mfululizo wa matukio ya watu kujiua nchini, wanaume wakiwa wengi zaidi, hali iliyozua gumzo miongoni mwa wananchi.

Wakati matukio hayo yakiendelea kutokea, Januari, 2021 ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), iliitaja Tanzania kushika nafasi ya 27 barani Afrika kwa vifo vinavyotokana na watu kujiua.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, ripoti hiyo inaonyesha kuwa Tanzania inashika nafasi ya nne kwa kuwa na idadi kubwa ya wanaojiua.

Katika ukanda huo, Rwanda inaongoza kwa kuwa na asilimia 8.5 ya vifo vya kujiua ikifuatiwa na Burundi yenye asilimia nane. Nafasi ya tatu inashikiliwa na Uganda kwa kuwa na asilimia 7.1 huku Tanzania ikishikilia nafasi ya nne kwa kuwa na asilimia saba.

Uwapo wa hali hiyo, umeifanya Nipashe kumtafuta mtaalamu wa saikolojia, John Ambrose, ili kufahamu sababu, namna ya kukabili hali hiyo pindi mtu inapomtokea.

Anasema wanaojiua huwa wanatafuta suluhu ya kumaliza tatizo lililo mbele yao.

Ambrose anasema ugumu wa maisha unachagiwa na majukumu aliyo nayo mtu kama kulipa ada ya watoto shuleni au chuoni, kodi ya nyumba na mahitaji mengine ya familia kuzidi uwezo wa kipato na kusababisha mtu kupata sononа.

Anasema liko suala la kuwezesha wanawake kiuchumi ambalo limeendelea kukua licha ya mila la desturi za Watanzania kutobadilika, majukumu kubaki upande wa mwanamume.

"Wanawake wanakua kiuchumi duniani, wanawezeshana na kuendelea kukua wakati huo huo mila na desturi hazijabadilika. Hali hii inasababisha wanaume kupata sonona na kujiua," anasema Ambrose.

Anabainisha zaidi kuwa wanaume kutokuwa na kipato cha kutosha wakati majukumu ya familia waliyo nayo ni makubwa kuliko kipato, husababisha kupata tatizo la afya ya akili.

"Wanawake wanashikilia uchumi lakini majukumu yote anaachiwa mwanamume. Hii inasababisha chuki, hasira na ugomvi ndani ya familia na matokeo yake wanandoa hutengana na hata kujiua," anasema.

Kuhusu ugonjwa wa akili anasema ni tatizo ambalo mtu anazaliwa nalo au anasababishiwa na msononeko wa muda mrefu ambao huchangia mtu kupata sonona.

Magonjwa ya akili kama sonona ni mawazo yaliyopitiliza na kusababisha mtu kujiua.

Anasema dalili kubwa za ugonjwa wa akili zinasabishwa na tatizo la kukojoa kitandani, kula kupita kiasi, kukosa usingizi na tabia zinazompa mtu aibu au fedhea ndani ya jamii yake. Ambrose anasema ugonjwa wa sonona unaongoza duniani na ni wa nane kwa kuua kwa njia ya kujirusha na kujinyonga.

### NINI KIFANYIKE?

Ambrose anasema utafiti wa kina unahitajika ili kufahamu sababu kuu zinazofanya watu kujiua.

Pia anasema jamii ipewe elimu ya kutosha kuhusu ugonjwa wa sonona na namna ya kuepuka ili kupunguza tatizo hilo kuendelea kukithiri nchini. Anasema pia watu wanatakiwa waelezwe ni sababu zipi zinamfanya mtu atamani kujiua hasa ikizingatiwa si suala la dharura humchukua muda mrefu hadi kufikia uamuzi huo.

Ambrose pia anashauri kuwa ili kuepuka tatizo hilo pia jamii inatakiwa kuepuka kubeba mambo mengi kuliko uwezo wao.

"Kumekuwapo na utaratibu wa watu kuishi maisha ya matarajio makubwa kuliko uwezo na kipato, tamaa na kuishi kwa imani badala ya kuishi kwa mipango waliyojiwekea," anasema.

Anasema jamii isibebe mambo mengi kuliko uwezo bali waishi kulingana na kiwango na uwezo husika ili kuepuka kupata tatizo la kutaka kujiua.

Mtaalamu huyo anashauri pia jamii kuweka utaratibu wa kufanya mazoezi ya mwili na viungo kwa sababu yanaratibu mfumo wa akili na kujiondoa kwenye hatari kubwa ya kupata magonjwa ya akili. Pia anashauri watu kuzingatia mpangilio wa chakula kwa kula milo kamili inayohitajika ndani ya mwili.

"Watu wengi siku hizi wanakula kwa kuzingatia mahitaji ya hisia zao za kutaka kupungua na si kwa sababu ya kukidhi mahitaji ya mwili," anabainisha.

Ambrose anasema pia watu wanatakiwa wapumzike na walale muda mrefu kwa sababu ni tiba na sehemu ya kupumzisha akili ili kuanza upya na kuweka bayana kuwa watoto kujiua kunasababishwa na kupata maudhi au kulia ndipo hufikia hatua hiyo.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (kushoto), akikabidhi msaada wa madawati 45 yaliyotolewa na Kampuni ya Bima ya Afya ya Jubilee kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kisutu, Elizabeth Massawe, jijini Dar es Salaam juzi kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo. Dr. Harold Adamson na wa pili kushoto ni Diwani wa Kata ya Kisutu, Abdulkher Kessy. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Historia yaandikwa ndege mizigo kutua nchini

**Na Jenifer Gilla**

NI historia imeandikwa baada ya jana Rais Samia Suluhu Hassan kupokea ndege mpya ya mizigo aina ya Boeng 5766-300F yenye uwezo wa kubeba tani 54 za mizigo kwa wakati mmoja.

Mapokezi ya ndege hiyo yalifanyika jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) majira ya saa 9:00 alasiri na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, dini na vyama vya siasa.

Sambamba na kupokea ndege hiyo, Rais Samia aliridhia ombi lililotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Ladislaus Matindi, la kutaka kununuliwa ndege nyingine ya mizigo kutokana na kuwapo uhitaji mkubwa wa soko la usafiri wa mizigo na kuifikisha ikiwa na ubora unaohitajika.

Aidha, Rais Samia aliwaomba Watanzania kuendelea kuwaombea viongozi wa serikali wapate nguvu ya kufanya kazi ili waendelee na shughuli mbalimbali za ujenzi wa taifa.

"Tumeombwa ndege nyingine hapa ya mizigo, ahadi yangu kwenu au ahadi yetu kwenu wananchi tutalifanyia kazi," alisema Rais Samia.

**MKURUGENZI ATCL**

Akiwasilisha ombi la kuongezewa ndege nyingine ya mizigo, Matindi alisema: "Kutokana na hali halisi la hitaji la usafiri wa mizigo, ambalo nitalielezea baadaye ni vyema ndege za mizigo zikawa mbili.

"Hivyo Mheshimiwa Rais tunaleta ombi letu kwako utuongezee ndege moja ya mizigo ili kukabiliana na hitaji la soko."

Matindi alisema tathmini ya utendaji wa ATCL katika soko la anga la usafirishaji mizigo nchini inaonyesha matumaini makubwa ya kukua kwa mwenendo wa usafirishaji wa mizigo kupitia ndege za abiria tangu utekelezaji wa mpango wa ufufuaji wa shirika hilo mwaka 2019.

Alisema walianza kubeba tani 334 mwaka wa fedha 2017/18 hadi tani 2,567 mwaka 2021/22 huku Julai, 2022 hadi Aprili, mwaka huu, imeshabeba tani 2,895.

Matindi alisema tangu shirika hilo kuanzishwa Septemba 2016, limerudishiwa uanachama wa mashirikisho ya mashirika ya ndege duniani, kufaulu ukaguzi wa kimataifa wa viwango vya usalama na uendeshaji wa usafiri wa anga.

Pia alisema limerudishwa katika mifumo ya kimataifa ya uendeshwaji wa utoaji wa huduma ya usafiri wa anga, kukaguliwa mahesabu yao na kupata hati safi ya CAG kuanzia mwaka 2017 hadi 2021/22.

Alisema vilevile ATCL imeongeza mtandao wa safari kutoka vituo vitatu hadi 14 ndani ya nchi na kutoka kituo kimoja hadi vituo 10 nje ya nchi, kuongeza marubani wazawa kutoka 11 hadi 105 kati ya hao 10 wakiwa ni wanawake.

Aidha, alisema usafirishaji wa mizigo kupitia ndege za abiria umekuwa haukidhi mahitaji ya soko kutokana na ufinyu wa nafasi za mizigo kwenye ndege hizo matokeo yake baadhi ya mizigo kutokusafirishwa na kuchelewa kufika sokoni na kulinyima shirika hilo mapato.

Alisema uwapo wa ndege hiyo, utasaidia kuongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa za Tanzania, kutaongeza thamani ya bidhaa na kuzifanya ziwe shindani zaidi katika soko la kimataifa.

Matindi alisema uwapo huo utaifanya Tanzania inufaike na fursa nyingi za usafirishaji wa mizigo zinazopatikana nchini kwenda nje ya nchi kama vile ikiwamo minofu ya samaki kutoka Kanda ya Ziwa, dagaa na samaki wa mapambo kutoka Ziwa Tanganyika, nyama, maua , matunda na mboga na mazao ya Baharini kutoka Zanzibar na Ukanda wa Bahari ya Hindi.

"Mazao haya ni rahisi kuharibika hivyo kufanya usafirishaji kwa njia ya anga kuwa sahihi zaidi ili kuhifadhi ubora wake yanapofika nchini sokoni," alisema.

Ndege hiyo, alisema kwa kuanzia itafanya safari zake katika miji ya Nairobi, (Kenya) Harare (Zimbabwe), Johannesburg (Afrika Kusini), Kinshansa (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) Lagos (Nigeria), Guangzhou (China), Mumbai (India) na Umoja wa Falme wa Kiarabu (UAE) huku ikiwa na matarajio ya kufanya safari za ratiba zisizo maalum zikiwamo katika Bara la Ulaya.

# Mwenyekiti matatani kushawishi wananchi kususia ujenzi wa shule

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Muragili, amemshtaki Mwenyekiti wa Kijiji cha Msimihi, Ramadhani Ally, kwa Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, kwamba amekuwa kikwazo kwa kuzuia wananchi kushiriki ujenzi wa Shule ya Msingi Murya.

Muragili aliwasilisha malalamiko hayo juzi baada ya Serukamba kufanya ukaguzi katika shule hiyo. Alisema kusuasua kwa ujenzi huo kumesababishwa na mwenyekiti ambaye anahamasisha wananchi wa vitongoji viwili wasishiriki nguvu kazi.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa nilikuja hapa Mei 20, 2023 kukagua nikabaini kikwazo katika mradi huu ni Mwenyekiti wa Kijiji ambaye alikuwa anazuia shule kujengwa hapa, lakini wewe niachie hili suala huyu ni saizi yangu nitapambana naye," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Ramadhani Ally, alipopewa nafasi ya kuongea alijibu kuwa hajapinga ujenzi wa shule isipokuwa eneo inapojengwa kulikuwa na mgogoro hali iliyosababisha mvutano wa wananchi wa vitongoji vinne vinavyounda kijiji cha Msimihi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba, alisema ni jambo la kushangaza kwa wananchi kutoshiriki nguvu kazi katika ujenzi wa shule hiyo wakati serikali imewarahisishia kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi huo.

Serukamba alisema ili miradi iweze kukamilika kwa wakati wakurugenzi wa halmashauri wawapangie wakuu wa idara kila mmoja kusimamia mradi mmoja inayotekelezwa hivi sasa na wawe wanatoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi kila siku, kwamba ikamilike kabla ya Juni 30 mwaka huu.

Alisema ujenzi wa miradi unasuasua katika baadhi ya halmashauri kwa sababu kazi ya kuisimamia wameachiwa walimu na kamati za shule.

Mkuu wa mkoa alisema hapendi kuona fedha zilizoletwa katika mkoa huu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zinarudishwa baada ya mwaka wa fedha kumalizika kwa kushindwa kukamilisha miradi. Kutokana na hali hiyo, aliagiza kila mkuu wa idara kukabidhiwa mradi wa kuusimamia ili ikamilike kabla ya Juni 30, mwaka huu.

'Walimu kazi wanayojua ni kufundisha tu hivyo kusimamia miradi mikubwa wanaweze wasimudu vyema jukumu hilo, hivyo iwapo wakuu wa idara watapewa kazi kuisimamia watasaidia kuweka mipango mizuri ya ujenzi na kuwa daraja kati ya halmashauri, mkuu wa wilaya na mkuu wa mkoa," alisema.

Serukamba aliambatana na Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, ambaye alisema serikali imepeleka fedha nyingi kwenye halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hivyo isimamiwe, wananchi waendelee kuhamasishwa kujitolea nguvu kazi.



# TLP yamtimua Mwenyekiti kisa utovu nidhamu

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Tanzania Labour Party (TLP), kimemfukuza uanachama Mwenyekiti wa Vijana wa chama hicho, Aivan Maganza, kwa tuhuma za utovu wa nidhamu.

Akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama hicho, Magomeni Usalama jijini Dar es Salaam juzi, Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo, alisema kamati ya chama hicho ndiyo uliochukua uamuzi huo.

Lyimo alitaja baadhi ya tuhuma zinazomkabili Maganza ni kuitisha mkutano na waandishi wa habari na kutukana viongozi wa chama hicho.

"Katika mazungumzo yake na waandishi wa habari pamoja na mambo mengine alitangaza tarehe ya uchaguzi wa mwenyekiti wa chama taifa kuwa ni Juni 18 mwaka huu," alisema Lyimo.

Alisema kwa sababu hiyo kamati ikaamua kuchukua hatua hiyo ya kumfukuza uanachama.

"Kamati ya nidhamu TLP taifa ilikutana na kupendekeza kwenye kikao cha sekretalieti ya chama kwamba hafai kuwa kiongozi wa TLP katika ngazi yoyote," alisema.

Lyimo alisema kikao hicho kwa idhini ambayo kimepewa na Katiba ya TLP, toleo la 2009, ibara ya 9.5 na ibara ya 18.9 (a), (b) na (d), kwamba kwa kauli moja kimekubaliana kumfukuza katika chama mwenyekiti huyo.

"Haruhusiwi kufanya au kuonekana katika ofisi yoyote ya TLP kuanzia ngazi ya taifa hadi shina, anaruhusiwa kukata rufaa kwa ngazi za juu zaidi za chama," alisema.

Akizungumzia uamuzi huo, Maganza alisema TLP haina kamati ya nidhamu kwa miaka mingi na kwamba hata kama ingekuwapo, haina uwezo wa kumfukuza katika chama.

Alisema kazi ya kamati hiyo kama ingekuwapo ingekuwa na wajibu wa kumuita, kumhoji na kutoa mapendekezo.

Aliongeza kuwa taarifa aliyotoa kwa waandishi wa habari na kusababisha kuwapo kwa taarifa hizo za kufukuzwa Iko palepele.



Mteja akichagua vyombo vya nyumbani katika soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali, UNESCO kuimarisha uchumi vyombo vya habari

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasilino na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) zimetia saini ya makubaliano ya ushirikiano kwa miaka mitano katika kuimarisha hali ya uchumi wa vyombo vya habari nchini.

Makubaliano hayo yanalenga kuangalia usalama na ulinzi sehemu ya kazi za waandishi wa habari, kuimarisha uchumi wa vyombo vya habari na uhuru wa habari, kutoa mafunzo ya kuwaendeleza wanahabari ili kutekeleza majukumu yao na kuimarisha mazingira ya kisera na sheria.

Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Nape Nnauye, alitia saini makubaliano hayo na UNESCO jana jijini Dar es Salaam.

Wakati wa hafla hiyo, Nape alisema makubaliano hayo yatasaidia vyombo vya habari kuimarika na kufanya kazi zao kwa ufanisi unaotakiwa.

"Tayari serikali imeshaanza mapitio ya sera na Muswada wa Sheria ya Habari ili kuwa na sheria inayokidhi mahitaji yetu," alisema Nape.

Aidha, alisema makubaliano hayo yanalenga kuimarisha mazingira ya habari kwa kutumia dijitali katika habari.

"Makubaliano hayo pia yamekuja baada ya kuona vyombo vya habari vingi vya Afrika vina matatizo katika utendaji wao wa kazi," alisema.

Naye Mkuu wa Ofisi na Mwakilishi wa UNESCO, Michael Toto, alisema tangu mwaka 2022 hadi 2027 wamelenga kuisaidia Serikali ya Tanzania kubaini matatizo mbalimbali ikiwamo kuziripoti na kuharakisha ili kufikia malengo endelevu.

Toto alisema makubaliano hayo yatafanya kazi maeneo matano ya kipaumbele kwa kushirikiana na wadau maeneo hayo.

Alisema: "Kuimarisha mazingira sehemu ya kazi ya wanahabari itasaidia kufichua mambo mengi ambayo hivi sasa hayajulikani na ndio maana tumeweka mafunzo ya wanahabari katika makubaliano yetu".

# Aweso atekeleza agizo la Katibu Mkuu CCM

**Na Nebart Msokwa,** KILOLO

MAAGIZO yaliyotolewa na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, kwa viongozi wa wizara mbalimbali kushughulikia matatizo ya wananchi mkoani Iringa, yameanza kutekelezwa.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ndiye amekuwa wa kwanza kwenda kuwasikiliza wananchi walioangua vilio mkoani humo wakilalamikia mradi wa maji kukwama kwa zaidi ya miaka 10.

Akiwa ziarani wilayani Kilolo, Chongolo alitembelea Kata ya Uhambingeto na kubaini mradi wa maji ambao serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 2.1 kwa ajili ya kuujenga ukiwa umekwama huku mkandarasi akidaiwa kuutelekeza na kutokomea kusikojulikana.

Wananchi wa kata hiyo wakiongozwa na diwani wao, Tulinumtwa Mlangwa, waliangua vilio huku wakimwomba Katibu Mkuu huyo kuwasaidia kuisukuma Wizara ya Maji ili mradi huo ukamilike na kuwaondolea kero ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Chongolo aliagiza Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kukamilisha ujenzi wa mradi huo ndani ya miezi mitatu ili kuwaondolea wananchi kero hiyo.

Juzi, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alifika katika kata hiyo kwa ajili kushughulikia tatizo hilo ikiwa ni siku tatu baada ya Katibu Mkuu kumpa siku 10 kwenda kushughulikia tatizo hilo. Akiwa katika eneo hilo, Aweso alikiri kwamba kuna uzembe ulifanyika kwenye usimamizi wa mradi huo.

"Wakati Rais Samia analihutubia Bunge alinisimamisha na kusema 'yeye ni mama hataki kuona wananchi wanateseka kwa sababu ya kukosa maji' nikimzingua atanizingua, na mimi sitaki kuzinguliwa na ndiyo maana nimekuja haraka kushughulikia tatizo hili," alisema Aweso.

Aliwaagiza watendaji wa RUWASA Mkoa wa Iringa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kila wiki mpaka utakapokamilika, huku akimwomba mkuu wa mkoa huo kuwashughulikia watendaji watakaozembea ikiwamo kuwasweka ndani.


Mbunge wa Kilolo, Justine Nyamoga, alisema kata ya Uhambingeto ni miongoni mwa maeneo kame zaidi katika jimbo hilo kutokana na vyanzo vya maji kuwa mbali.

Alisema wananchi wamekuwa wakipata shida zaidi kipindi cha kiangazi ambacho huwa wanalazimika kununua maji kwa bei kubwa. Nyamoga alisema hali hiyo imekuwa ikiwasababishia magonjwa mbalimbali yakiwamo magonjwa ya matumbo, hivyo akaiomba serikali kuharakisha mradi huo ili kuwaondolea tatizo hilo.

Mwakilishi wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Maji na Mazingira ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Iringa, Ritta Kabati, alisema tatizo la maji katika eneo hilo limekuwa likisababisha ndoa kuwa hatarini kuvunjika kutokana na wanawake kutumia muda mrefu kutafuta maji.

Alisema wamekuwa wakiamka usiku kwenda kutafuta huduma hiyo hali ambayo pia inahatarisha maisha yao na hivyo akaiomba serikali kuharakisha mradi huo kukamilika.

Diwani Mlangwa alisema mradi huo ukikamilika utawanufaisha wananchi 12,000.



Kaimu Mkurugenzi wa jiji la Dar es Salaam, Mhandisi, Amani Mafuru (kushoto), akibadilishana mkataba na Mkandarasi wa Kampuni ya Southern Link Limited, Johnbosco Mosha, wakati wa kusaini mkataba wa ujenzi wa barabara kilomita 1. 2 katika Wilaya ya Ilala juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwenyekiti matatani kuhamasisha wananchi wasishiriki ujenzi wa shule

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Muragili, amemshtaki Mwenyekiti wa Kijiji cha Msimihi, Ramadhani Ally, kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, kwamba amekuwa kikwazo kwa kuzuia wananchi wasishiriki ujenzi wa Shule ya Msingi Murya.

Muragili aliwasilisha malalamiko hayo juzi baada ya Serukamba kufanya ukaguzi katika shule hiyo.

Muragili alisema kusuasua kwa ujenzi huo kumesababishwa na mwenyekiti ambaye anahamasisha wananchi wa vitongoji viwili wasishiriki nguvu kazi.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa nilikuja hapa Mei 20,2023 kukagua nilibaini kikwazo katika mradi huu ni Mwenyekiti wa Kijiji ambaye alikuwa anazuia shule isijengwe hapa, lakini wewe niachie hili suala huyu ni saizi yangu nitapambana naye," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Ramadhani Ally alipopewa nafasi ya kuongea alijibu kuwa hajapinga ujenzi wa shule isipokuwa eneo inapojengwa kulikuwa na mgogoro hali iliyosababisha mvutano wa wananchi wa vitongoji vinne vinavyounda Kijiji cha Msimihi.

Mkuu wa Mkoa Singida, Serukamba alisema ni jambo la kushangaza kwa wananchi kutoshiriki nguvu kazi katika ujenzi wa shule hiyo wakati serikali imewarahisishia kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi huo.

Serukamba alisema ili miradi iweze kukamilika kwa wakati wakurugenzi wa halmashauri wawapangie wakuu wa idara kila mmoja kusimamia mradi mmoja inayotekelezwa hivi sasa na wawe wanatoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi kila siku, kwamba ikamilike kabla ya Juni 30 mwaka huu.

Alisema ujenzi wa miradi unasuasua katika baadhi ya halmashauri kwa sababu kazi ya kuisimamia wameachiwa walimu na kamati za shule.

Alisema hapendi kuona fedha zilizoletwa katika mkoa huu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zinarudishwa baada ya mwaka wa fedha kumalizika kwa kushindwa kukamilisha miradi.

Hivyo, aliagiza kila mkuu wa idara kukabidhiwa mradi wa kuusimamia ili ikamilike kabla ya Juni 30, 2023.

"Walimu kazi wanayojua ni kufundisha tu hivyo kusimamia miradi mikubwa wanaweze wasimudu vyema jukumu hilo, hivyo iwapo wakuu wa idara watapewa kazi kuisimamia watasaidia kuweka mipango mizuri ya ujenzi na kuwa daraja kati ya halmashauri, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa," alisema.

Serukamba aliambatana na Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, alisema serikali imeleta fedha nyingi kwenye halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hivyo isimamiwe, wananchi waendelee kuhamasishwa kujitolea nguvu kazi.

# Kiama chaja wanaotiririsha majitaka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, ameliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuwachukulia hatua wananchi wanao tiririsha maji taka kwenye mitaro ya barabara.

Alitoa agizo hilo jana mkoani hapa wakati akizungumza na wakazi wa Jiji la Dodoma baada ya kufanya usafi katika eneo la Mji Mpya ikiwa ni sehemu ya kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mazingira Dunuani.

Alisema wakati akishiriki kufanya usafi katika mitaa ya barabara ya saba, nane na tisa amebaini kuwa mitaro mingi ambayo imejengwa maalum kwa ajili ya kupitisha maji ya mvua wakati wa masika watu wanaitumia vibaya kwa kutiririsha maji taka.

"Niwaagize NEMC kufanya ukaguzi wa uchafuzi wa mazingira jijini Dodoma hasa kwa watu hawa ambao wamekuwa wakitiririsha maji taka kwenye mitaro hii iliyojegwa na kwa yeyote atakayebainika achukuliwe hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine,"alisema Ndejembi.

Aidha, aliwataka wakazi wa Jiji la Dodoma kuendelea kufanya usafi kila wakati badala ya kuendelea kusubiri hadi siku za maadhimisho kama hayo.

Kadhalika aliwataka viongozi wa mitaa, vitongoji,vijiji pamoja na kata kuhamasisha wananchi kushiriki kufanya usafi kila jumamosi ya mwisho wa mwezi ili kuendelea kuhifadhi mazingira.

"Niagize pia halmashauri zote nchini kila wanapopima viwanja wahakikishe kuwa wanapanda miti ili kufanya maeneo yote kuwa ya kijani lakini pia maeneo mengi ya wazi ambayo hivi sasa ni vumbi tupu yapandwe miti kama ilivyokuwa hapo zamani wakati tunayo Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA), ambao walikuwa wana utaratibu wa kupanda miti katika maeneo ya mji na kuitunza"alisema

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Godwin Gondwe, alisema wameanza kutekeleza maagizo ya serikali ya kuwa na kitalu cha miti na kwa kuanzia wametenga Sh. milioni 20 kwa ajili ya kustawisha miche ya miti na kuipanda katika maeneo mbalimbali.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema wiki hii watanza utaratibu wa kukaguma maeneo mbalimbali ya mji na watakapo baini watu wanachafua mazingira hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

# MUHAS waomba kupewa Muhimbili

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Baraza la Chuo Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), Dk. Harrison Mwakyembe, amemwomba Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kuirejesha Hospitali ya Muhimbili- Tawi la Mloganzila kuendelea kuwa chuo cha kujifunzia kwa vitendo.

Alitoa ombi hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza kwenye mkutano wa mafunzo yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).

Mafunzo hayo yalishirikisha wenyeviti wa mabaraza wa vyuo vikuu, wajumbe wa mabaraza, seneti na bodi za vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki nchini yakiwa na lengo la kubadilisha uzoefu wa namna bora ya kuviendesha.

Dk. Mwakyembe alisema MUHAS ilitafuta eneo Mloganzila kwa ajili ya kujenga hospitali ya kujifunzia kwa vitendo na kuhakikisha wanatoa elimu shirikishi.

"Maprofesa wa MUHAS walisimamia kikamilifu kuhakikisha wanatafuta fedha za ujenzi wa majengo yakakamilika. Mloganzila siyo hospitali ya kawaida ini kwa ajili ya wanafunzi wa udaktari kujifunza lakini kwa bahati mbaya serikali imeifanya kuwa Hospitali ya MNH," alisema Dk. Mwakyembe.

Alisema tayari wameshamwandikia barua Rais Samia Suluhu Hassan kuomba kurejeshewa hospitali hiyo na tume imeshaundwa kufanyia kazi suala hilo.

"Tukirudishiwa hospitali yetu tuliyojenga wenyewe, naamini MUHAS itafanya vizuri zaidi na kushika nafasi ya 10 bora duniani kwa ubora wa elimu. Naomba sana Waziri Prof. Mkenda kutusaidia kuturudishia hospitali yetu," alisema Dk. Mwakyembe.

Naye Prof. Mkenda, akijibu hoja hiyo alisema suala hilo linafanyiwa kazi na tayari limefika pazuri na majibu yatapatikana hivi karibuni.

Mbali na hilo Prof. Mkenda alikemea tabia ya baadhi ya vyuo vikuu nchini kutumia utafiti kama chanjo cha mapato.

Alikitolea mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambacho kimekuwa kikikusanya asilimia 30 ya fedha za kufanya utafiti kama mapato ya chuo na hivyo kupunja fedha zinazofanyia tafiti.

"Nimeshasema hili na leo nalirudia tena kwenye hadhira hii, vyuo sio TRA (Mamlaka ya Mapato) kukusanya asilimia 30 ya mapato wanayokusanya kwa ajili ya kufanya utafiti mnakosea, mnasababisha kupunja nauli za watafiti walizotakiwa kulipwa, na kuwapa vikwazo vya kushindwa kukamilisha utafiti," alisema Prof. Mkenda.

Pia alisisitiza utoaji wa elimu ya vyuo vikuu yenye tija kwa taifa badala ya kuangalia maslahi binafsi au ya vyuo kwa sababu hatari yake ni kuzalisha wataalamu ambao siyo msaada kwa jamii.

Prof. Mkenda pia alikemea urasimu wa kukwamisha safari za watumishi wa vyuo vikuu wanaoenda nje ya nchi kujifunza mambo mbalimbali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ndege mpya ya mizigo ilete mageuzi kiuchumi

**TANZANIA** jana iliandika historia ya aina yake baada ya kutua kwa ndege kubwa ya mizigo ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) aina ya Boeng 5766-300F yenye uwezo wa kubeba tani 54 za mizigo kwa wakati mmoja. Mapokezi ya ndege hiyo yalifanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam huku Rais Samia Suluhu Hassan akiwa mgeni rasmi.

Kuwasili kwa ndege hiyo ambayo itabeba mizigo na kusafirishwa sehemu mbalimbali duniani zikiwamo nchi za jirani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), India, China katika jiji la kibiashara la Guangzhou, kunaonyesha nia njema ya serikali ya kuleta mageuzi ya kibiashara ndani ya nchi.

Ndege hiyo, itawezesha sasa wafanyabiashara ambao wamekuwa wakiagiza mizigo kutoka na pia kupeleka sehemu mbalimbali kupata unafuu mkubwa kutokana na changamoto walizokuwa wakizipitia.

Kabla ya ujio wa ndege hiyo, wafanyabiashara wengi walikuwa wakitumia ndege za abiria na chache za mizigo na hata kusababisha ucheleweshaji mkubwa wa mizigo au kufika ikiwa katika hali mbaya. Lakini sasa, kuwapo kwa ndege hiyo kutawawezesha kusafirisha mizigo kwa wakati na kufika sokoni kwa unafuu mkubwa.

Hivi karibuni, mathalan, wazalishaji na wadau wa kilimo cha mboga na matunda, walisikika wakilalamikia tatizo la usafiri wao kutoka nchini kwenda kwenye masoko. Kwa mantiki hiyo, kuwasili kwa ndege hiyo ni ukombozi kwao kwa kuwa watapata fursa ya kusafirisha bidhaa zao kwa urahisi na kwa unafuu na matokeo yake watapata faida kwa kuwahi sokoni.

Ni faraja kubwa kwamba baada ya kuwasili kwa ndege hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alitoa ombi kwa serikali kuongeza ndege nyingine ya mizigo ambalo lilikubaliwa na Rais Samia . Ombi hilo lilitokana na ukweli kwamba hivi sasa kuna uhitaji mkubwa wa soko la usafiri wa mizigo na kuifikisha ikiwa na ubora unaohitajika.

Ni dhahiri kwamba usafiri wa anga ni wa haraka na wa kuaminika katika kusafirisha abiria na mizigo kwa wakati tofauti na aina zingine za usafiri. Kuwapo kwa ndege mpya ya mizigo na ile itakayonunuliwa kutokana na Rais kuafiki ombi la ATCL, kutarahisisha usafiri wa mizigo ndani na nje ya nchi, hivyo kuchangia kukua kwa uchumi.

Hivi sasa, kwa mfano, mfanyabiashara wa Dar es Salaam anayeagiza samaki kutoka Mwanza, huchukua siku kadhaa hadi mzigo kufika na hata ukifika unakuwa katika ubora tofauti kwa kuwa unasafirishwa kwa treni au magari na huchukua muda mrefu hadi kufika.

Kutokana na uwapo wa ndege ya mizigo, sasa mzigo utafika ukiwa katika ubora kwa kuwa utasafirishwa ndani ya saa chache kutoka Mwanza hadi Dar es Salaam. Kwa mantiki hiyo, watumiaji wengi wa vitoweo vya samaki mkoani Dar es Salaam, kutokana na ujio wa ndege hiyo, watakula vitu ambavyo ni vya uhakika.

Tunasema ni vya uhakika kwa sababu kutoka Mwanza hadi Dar es Salaam, Samaki wamekuwa wakigandishwa kwenye barafu na wakati mwingine kuwapo dhana kwamba wamekuwa wakiwekewa dawa za maiti.


Aidha, uwapo wa ndege hii kubwa utafungua milango kwa wafanyabishara kusafirisha nyama na bidhaa zingine ambazo zinahitajika katika masoko mbalimbali kama vile UAE na Comoro ambako kuna uhitaji mkubwa wa nyama ya mbuzi na ng'ombe.

Kwa jambo hilo serikali inastahili pongezi kubwa na imeonyesha dhamira ya dhati katika kukuza uchumi na pato la taifa kwa ujumla. Sasa kazi kwa wafanyabiashara kuchangamkia fursa ya uwapo wa ndege hiyo ambayo ni Imani kwamba itakuwa na unafuu wa gharama kulinganisha na ndege za mashirika ya kimataifa.

Jambo la msingi ni kwamba utunzaji na matumizi ya ndege hiyo uwe na tija katika kuleta mageuzi ya kibiashara na kiuchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Itikadi za vyama ni kigingi kufikia usawa wa kijinsia

**USAWA** wa kijinsia ni miongoni mwa mambo ambayo wanaharakati wamekuwa wakitamani, ili kuhakikisha idadi ya wanawake inakuwa sawa na ya wanaume katika uongozi na kwenye ngazi mbalimbali.

Hata hivyo, kumekuwapo na mtazamo kwamba wanawake hawapendani, kutokana na itikadi za vyama, hali ambayo kwa namna moja au nyingine inaweza kusababisha kuwa kikwazo kufikia usawa wa kijinsia.

Kama suala la itikadi za vyama linapewa nafasi ya kuvuruga ushirikiano wa wanawake na kushindwa kufikia usawa wa kijinsia, ni vyema wakalitazama kwa umakini na kulitafutia ufumbuzi.

Ikumbukwe kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, hivyo itikadi za vyama zingewekwa pembeni ili kama kuna mwanamke ambaye anafaa kupewa nafasi ya uongozi, basi achaguliwe bila kujali itikadi.

**Ikumbukwe kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, hivyo itikadi za vyama zingewekwa pembeni ili kama kuna mwanamke ambaye anafaa kupewa nafasi ya uongozi, basi achaguliwe bila kujali itikadi.**

Pamoja na suala la itikadi za vyama, kumekuwapo pia na madai kwamba wanawake hawapendani, sababu kubwa ikiwa ni kuoneana wivu wa kutokana mwingine apate nafasi ya uongozi. Ninaamini kwamba iwapo mtindo huo wa kuzingatia itikadi za vyama utaendelea na kuoneana wivu, inaweza kusababisha wanawake wakasubiri sana kufikia usawa wa kijinsia wanaoutamani.

Lakini pamoja na mkakati wa kutaka usawa wa kijinsia, ninadhani kuna haja ya kuwapa angalizo ili wazingatie kuepuka kuongeza wingi wa wanawake katika nafasi za uongozi bila kuangalia uwezo wa kuongoza.

Ingependeza kama wakapata wanawake wenye uwezo wa kuongoza na ushawishi, siyo kuwa na idadi kubwa tu ambayo haina manufaa, kwani lengo ni kupata uwakilishi au uongozi unaoleta matokeo chanya.

Ikumbukwe, Rais Samia Suluhu Hassan, ameshaweka wazi kuwa anateua kulingana na elimu ya mtu na uwezo wake wa kuongoza, si vinginevyo na anataka kila mwanamke kutambua hilo na kulifanyia kazi.

Jitihada za kuelekea usawa wa kijinsia katika uongozi zimeonekana baada ya Rais Samia kuchukua nchi, hivyo bado zinahitajika nyingine zaidi kutoka kwa wanawake wenyewe.

Jitihada zinazohitajika kutoka kwa wanawake ni kupendana, kuacha kubaguana kwa itikadi za vyama, lakini pia kuhakikisha wanachagua wenzao wenye uwezo wa kuongoza, si mradi mwanamke.

Kimsingi, uongozi si misuli, ni akili, busara na hekima, ambavyo vyote ni wazi wanawake wanavyo kama ilivyo kwa wanaume, hivyo jambo la muhimu ni wao kuhakikisha wanakuwa wamoja.

Semina, warsha na makongamano ya pamoja vinaweza kusaidia kuwaunganisha na kufanya jambo ikiwamo kuchaguliwa katika uchaguzi mkuu au wa serikali za mitaa, kwa kutambua kuwa wao ni jeshi kubwa.

Wingi wao unaweza kuwafanya wakapata nafasi nyingi katika uchaguzi kupitia wingi wao, kwani kwa kutumia wingi huo, hawatabaki kuwa wapigakura tu bali wagombea wanaochaguliwa.

Kwa njia hiyo, hawatakuwa tayari kubebwa katika kutafuta nafasi za uongozi, kwani kwa ubebwaji huo, baadhi yao hujikuta wakiingizwa katika rushwa ya ngono ili wapate uongozi.

Mmoja wao alishawahi kutamka kuwa wanawake wanapendana, lakini unapofika wakati wa uchaguzi wanatengana huku wengine wakikubali kutoa au kupokea rushwa na kukwamisha juhudi zao za kutaka kufikia usawa wa kijinsia. Ninadhani sasa ni wakati wa kubadilika.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Wosia wa Le Mutuz kwa CCM, serikali, wabunge na wapinzani



Pascal Mayalla

KAMA nilivyoahidi wiki mbili zilizopita kuwa nitawaandikia kile alichokisema mtoto wa Mzee Malecela, William Malecela kwa jina maarufu Le Mutuz katika mahojiano yetu na mimi ambayo hayakupangwa, ni mtu mnakutana tu unampiga maswali bila kumtayarisha. Le Mutuz ametangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi.

Kwa kawaida sisi waandishi wa habari tunapotaka kufanya mahojiano ya kihabari na mtu yeyote, huwa tunamwandaa na wakati mwingine hata kumtumia maswali ili aandae majibu.

Waandishi pia tumegawanyika. Wako waandishi wa maswali rahisi rahisi na waandishi wa maswali magumu. Ikitokea mwandishi wa maswali magumu umekutana na mtu bila kupanga ukampiga maswali magumu na akakujibu kwa ufasaha kama Le Mutuz, hiyo maana yake Le Mutuz ni akili kubwa. Kuna viongozi wengine akisikia tu anatafutwa na waandishi wa maswali magumu, anaingia mitini. Au kwenye mkutano na waandishi wa habari, mwandishi wa maswali magumu akiuliza swali gumu, kiongozi analikwepa kiaina.

Mahojiano na Le Mutuz, nimeiita wosia kwa sababu hakujiandaa na akatema nondo nzito. Mahojiano hayo yako kwenye mtandao wa YouTube na hapa nakuletea sehemu tu ya kwenye wosia wake. Nitaweka msisitizo ndani ya parandesi.

**PM ni Pascal Mayalla na WM ni William Malecela**

**PM:** Katika pita pita yangu, nimekutana na mwana JF wenzetu atajitambulisha.

**WM:** (Anacheka huku anatafuna bigijii) "Ha ha ha, Naitwa William John Samwel Malecela ni member wa JamiiForums, ni mmoja wa waanzilishi. Nimekuwa mwanachama toka tulipoianzisha na ninaipenda.

**PM:** Kuna mtazamo mtandao wa jamiiforums, kazi yake ni kulalamika tu, kuikosoa serikali, haueleze mazuri yoyote ya serikali, wao kazi yao ni kuvurumisha tuu makombora na ukosoaji, kuna ukweli kuhusu hili?".

Wosia kwa serikali: Serikali inatakiwa kufanya mema kwa wakati wote.

**WM:** Naomba kusema serikali yetu kwa muda mrefu imekuwa serikali ya chama kimoja. Sasa ukafika wakati tukaingia kwenye vyama vingi, wakati wote wa mfumo wa chama kimoja, wananchi walikuwa na madukuduku ya kutoa matatizo yao na serikali, haikuwapa nafasi. Tulipoingia vyama vingi wananchi wamepata nafasi ya kukosoa serikali, Jamiiforums hakipawi kuwa chombo cha kusifia serikali kinatakiwa kuwa chombo cha kukosoa serikali. Serikali kisheria by the law, inatakiwa kufanya mazuri wakati wote.

Wosia kwa Wabunge: Wasipoteze muda kuwasifu viongozi wao kwa kutimiza wajibu wao. Hakuna sababu ya sisi wananchi kuisifia serikali kwa mazuri inayoyofanya, kama juzi mbunge mmoja alipouliza Bungeni, haelewi ni kwa nini wabunge wengi wanapoteza muda wao kuwasifia viongozi wa vyama vyao Bungeni kwa mambo waliyoyafanya nje ya Bunge, huo ni wajibu wao.

Wosia kwa Jamiiforums, Mitandao, na Makundi Sogozi.

Jamiiforums inatakiwa kuwa chombo cha kuikosoa serikali, kuisaidia serikali kwa sababu serikali ni kubwa mno haiwezi kujiona kwenye kila kona ya mwili wake. Jamiiforums inaisaidia serikali kuona mapungufu yake lakini jamiiforums si mtandao wa CHADEMA. Nimesikia hizi habari siku nyingi kwamba jamiiforums ni mtandao wa CHADEMA, hapana! Mimi ni CCM, nimesema mara nyingi 'commitment' yangu ni kuhakikisha kuwa CCM inatawala kwa miaka 50 ijayo".

**PM:** Watanzania wameamka, hakuna chama cha kutawala milele?.

**WM:** Wosia kwa CCM: CCM ina tatizo la viongozi kwa viongozi wananchi hawana tatizo na CCM. Nimesema hivi, baada ya mkutano wa Jangwani nikashuhudia jinsi wale wananchi waliominika pale uwanjani, nikamwambia Mwenezi wa CCM Nape, tatizo la CCM ni sisi viongozi kwa viongozi.

Pamoja na mabaya yote yanayosemwa kuhusu CCM, CCM bado inapendwa na wananchi wa kawaida, umati wa watu uliojitokeza Jangwani bila kulazimishwa ni ushahidi wananchi hawana tatizo na CCM.

Wosia kwa CCM na Wapinzani: Siasa si uadui. Siasa si ugomvi, nimelithibitisha hilo kwenye mechi ya wabunge wa Yanga na wabunge wa Simba. Siasa si ugomvi, siasa inatakiwa kukosoana na kuelezana ukweli.

Ninasema CCM ina uwezo wa kutawala miaka 50 ijayo kama itajifunza kusikiliza, CCM haisikilizi. CCM wa 'introduce time limit' kwa uongozi ndani ya chama ili kuleta akili mpya, mawazo mapya.

Jana nimeshiriki kugombea ngazi ya kata, wilaya na mkoa, nilishtushwa kukuta watu walioshika vyeo kwa miaka 20, bado wanagombea, hawataki kutoka. Hilo ni tatizo kubwa la CCM, CCM lazima tufike mahali tuwekeane ukomo baada ya miaka 10 au 15, usigombee tena. Tupishe wengine, tulete akili mpya.

Wosia kwa Jamiiforums

Jamiiforums waendelee kuisaidia serikali kama inavyofanya sasa.

Wosia kwa CCM

CCM imekaa madarakani kwa muda mrefu sana inajisahau. Serikali inafika mahali inalala usingizi, serikali ni kubwa mno na tumetawala kwa muda mrefu sana (wosia kwa serikali, isilale usingizi). Watu wenye akili nyingi wanasema, ukikaa madarakani kwa muda mrefu sana, unafika mahali unajisahau. CCM kuna maeneo mengi tumeshaanza kujisahau, lakini 'we are alright', sawa Bwana Paskali.

Ni maneno makubwa mazuri, mazito aliyotuachia. RIP William Malecela 'Le Mutuz', wa kukuishi, watakuishi. Wasipotokea wewe umetimiza wajibu wako, mwendo umeumaliza kikamilifu.

**Wasalaam**
**Paskali.**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mnaopinga kazi inayofanywa na NEMC tuacheni



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

ZAMANI madarasani kulikuwa na mtu ambaye alikuwa mashuhuri sana na tukimwita 'monita (monitor)' ambaye alikuwa kiongozi wa darasa akiwa na kazi kubwa ya kudhibiti nidhamu ya wanafunzi, akimsaidia mwalimu wa darasa au wa somo.

Nje ya darasa kulikuwa na watu tunawaita 'maprifekti (prefects)' wakiwa chini ya 'mahedi prifekti (head prefects)' ili mradi muundo ulikuwa sawa na wa serikali, ambapo kuna mawaziri na waziri mkuu.

Tukirudi darasani, kazi kubwa ya monita ambaye baadaye Kiswahili kilipostawi zaidi akaja kujulikana kama kiranja wa darasa, ilikuwa hasa kusimamia wapiga kelele, akiwaandika majina na kuwasilisha kwa mwalimu husika kwa ajili ya kudhibiti nidhamu.

Kwa kweli hakuna jambo linalochukiwa shuleni tangu enzi hizo kama kelele darasani na lengo lilikuwa kuhakikisha kuwa kelele za darasa moja hazisababishi kero na kuingilia mafundisho ya darasa lingine.

Hivyo, ilikuwa bora kabisa mpige kelele darasani zisisikike kwa darasa lingine kuliko vinginevyo, na ndiyo sababu wapiga kelele waliadhibiwa vikali, ingawa tatizo hilo lilikuwa vigumu kulidhibiti.

Kutokana na hilo, ieleweke na kukumbukwa kuwa kelele ni chukizo la miaka mingi na ndiyo sababu hata leo mtu akipiga kelele bila sababu, huingizwa katika kundi la hamnazo, wendawazimu au vichaa na ikizidi hutafutiwa tiba hospitalini au kwa kina sangoma.

Imekuwa hivyo na sasa kimataifa kelele zinachukuliwa kama uchafuzi wa mazingira hata kuundiwa vyombo vya kuhakikisha kuwa makelele katika jamii yanadhibitiwa kwa kutungiwa sheria, ili kuhakikisha mazingira yanaendelea kuwa safi na salama.

Inapozungumzwa kelele kuwa uchafuzi wa mazingira, kinachozingatiwa ni afya ya apigiwaye kelele, mathalan mgonjwa hastahili kupigiwa kelele, kwani humsababishia maumivu zaidi na hata kumwondolea maisha.

Mtoto anastahili kupumzika, hivyo akipigiwa kelele anaweza asilale kwa muda mrefu na hivyo kuathiri afya na makuzi yake, vivyo hivyo katika kujiandaa kimasomo, kwamba mwanafunzi anastahili utulivu ili kujiandaa.

Palipo na kelele kuwa zisizo za lazima hapana utulivu na hivyo hapawezekani jambo kufanyika hususan linalohitaji utulivu, kama vile kujadili mambo ya maendeleo katika jamii au hata familia. Ndiyo sababu hata redio mtu hutakiwa kufungulia kwa kiasi.

Tanzania si kisiwa katika dunia hii, inaendana na taratibu zote za dunia katika kulinda na kuhifadhi mazingira, ikiwa ni pamoja na mazingira yanayotibuliwa na kelele na ndiyo sababu ikaamua kuunda Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Awali, baraza hili lilikuwa likipambana na uhifadhi wa mazingira hususan katika uchafuzi kwa majitaka lakini pia ukataji miti na mmomoyoko wa ardhi likijikita zaidi katika maeneo ya makazi ya watu mijini na vijijini.

Wakati wote huo, baraza lilipiga kazi bila malalamiko makubwa na likiungwa mkono na watu wengi kwamba lilikuwa linalinda maisha ya watu kabla halijaingia kwa nguvu kubwa katika hili la kelele au sauti kuwa na hata kufunga baadhi ya maeneo yaliyokithiri na yenye usugu wa kutozingatia sheria.

Ilipotangazwa hivi karibuni kwamba NEMC imefungia baadhi ya baa, ndipo moto ukalipuka kutoka maeneo mbalimbali kuiunguza NEMC kwa madai kuwa imefanya uonevu wa kufunga baa zinazopiga kelele kana kwamba wanaolalamika hawajui sheria!

Mshangao mkubwa ni pale hata baadhi ya wakuu wa mikoa walipoamua kuinanga NEMC, kwamba ilichokifanya ni kinyume hata baadhi wakadiriki kutangaza kufungulia waliofungiwa kwa kukiuka sheria za mazingira.

Wengine wakafikia kutamka kuwa bia haiwezi kunyweka sehemu yeye utulivu na kuwataka wasiotaka kelele wahame! Duh, sawa na yule aliyesema kama hamtaki tozo hamieni Burundi! Jamani hivi hii nchi tunakopelekwa ni wapi!

Kuwaacha viongozi wa aina hii kukwamisha na kutweza juhudi za baraza la mazingira ni kulikosea haki, lakini pia ni ukiukaji wa sheria kwa makusudi na hata kudharau Bunge linalotunga sheria kwa niaba ya wananchi.

Viongozi kama hawa hawajui nini maana ya utawala bora na utawala wa sheria, hivyo wanastahili kuonywa kama si kuondoshwa huku NEMC ikiongezwa meno na kugeuzwa kuwa Mamlaka kamili, ili iweze kufanya kazi kifua mbele.

Watanzania tukatae kelele kwenye baa, majumba ya ibada na kwingineko ili tulinde afya na mazingira yetu na kuishi kama binadamu na si kama wanyama ambao hata hivyo nao huogopa kelele seuze sisi binadamu! Tuiache NEMC ipige kazi tuache inda, wivu na tamaa!

**Alamsiki!**

# CBE kufundisha fani kwa soko la ajira

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) kuanzia mwaka huu wa masomo, kimepanga kuwapa wanafunzi ujuzi na maarifa muhimu katika fani zinazoendana na soko la ajira.

Fani hizo ni za ujasiriamali, uvumbuzi, uchumi, fedha, usafirishaji, usimamizi wa vifaa na masoko kidigitali

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Tandi Lwoga, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati akitambulisha kozi mpya ambazo zitaanza kutolewa katika mwaka wa masomo utakaoanza Oktoba, mwaka huu.

Alisema programu hizo mpya zitajumuisha kozi za vyeti vya ufundi wa msingi vyeti vya ufundi, shahada za kwanza, na shahada za uzamili.

Prof. Lwoga alisema CBE inajivunia kuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu ya biashara ya hali ya juu kwa miaka 58 sasa, inayokidhi mahitaji ya soko la ajira na kukuza ujasiriamali nchini.

Alisema kozi hizo ni matokeo ya utafiti za kina na jitihada za muda mrefu zilizofanywa na timu ya wahadhiri pamoja na wadau mbalimbali waliobobea katika tasnia husika.

Kozi hizo, alisema zinakusudia kutoa ujuzi wa vitendo, maarifa ya hali ya juu na mafunzo ya kina kwa wanafunzi wa chuo hicho ili kuwawezesha kufanikiwa katika soko la ajira na kukabiliana na matatizo.

Alitaja kozi hizo kuwa ni za vyeti vya ufundi wa msingi ambazo zitajumuisha, ujasiriamali na ubunifu, uchumi na fedha, usafirishaji na utafutaji masoko kidijitali.

Pia alisema chuo kitatoa shahada za kwanza katika ujasiriamali na ubunifu, usafirishaji, uchumi na fedha na shahada za uzamili kwenye usimamizi wa miradi tathmini na usimamizi.

Alisema kupitia Mradi wa Maendeleo Endelevu Kiuchumi (BUSEDA), CBE itaanza kutoa mtandaoni au kozi ya kupitia mtandao kwa wanafunzi wote wa shahada za uzamili ambayo itawapa ujuzi maalum kuhusu fursa za uwekezaji na biashara kwa ajili maendeleo ya kiuchumi katika nchi washiriki ambazo ni Finland pamoja na nchi tano za Afrika, ambazo ni Mauritius, Shelisheli, Malawi, Lesotho na Botswana. Kwa mujibu wa Prof. Lwoga, kozi hiyo inafadhiliwa na taasisi iitwayo Team Finland Knowledge Programme ambayo ipo chini ya Finnish National Agency for Education nchini Finland.

"Kozi hii inalenga kukuza uhusiano wa kibiashara, ujasiriamali, na uwekezaji kati ya Afrika na Finland na itatolewa kwa wanafunzi wote wa Shahada ya Uzamili kupitia mtandaoni ikiwa ni mara ya kwanza," alisema.

Prof. Lwoga alisema wanafunzi wataweza kujifunza fursa mbalimbali za kibiashara na jinsi ya kuwekeza Tanzania.

Alisema kuzinduliwa kwa kozi hizo mpya ni hatua muhimu katika kuongeza ubora wa elimu, kwamba wanaamini kuwa programu hizo zitawawezesha wanafunzi kuwa na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.



Kamishna Msaidizi wa Polisi Wilaya ya Kinondoni ACP, Ally Wendo, akizungumza na wakazi wa Kigogo jijini Dar es Salaam hivi karibuni wakati wa Kongamano la kupinga ukatili wa kijinsia lililoandaliwa na Taasisi ya Tanzania Ithna'ashariyah Community T.I.C. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JKT yakemea taarifa za uzushi mafunzo kwa mujibu wa sheria

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limekanusha taarifa zilizopo katika mitandao ya kijamii kwamba katika kambi za jeshi hilo kuna unyanyasaji wa kijinsia kwa vijana wanaoripoti kwa ajili ya mafunzo kwa mujibu wa sheria.

Mafunzo hayo kwa mujibu wa sheria yanatarajiwa kuanza mwezi huu katika kambi mbalimbali za jeshi hilo zilizopo katika mikoa tofauti hapa nchini.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Tawi la Utawala JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena wakati akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari.

Brigedia Jenerali Mabena alisema kumekuwa na taarifa za uzushi katika mitandao ya kijamii ambayo inaonyesha vijana wa kike wanafanyiwa ukatili wa kijinsia pale wanapokuwa katika mafunzo hayo ambayo hutolewa kila mwaka kwa lengo la kuwajengea uwezo pamoja na uzalendo kwa ajili ya nchi yao.

"Hakuna unyanyasaji wowote unaofanywa katika kambi za jeshi wakati wa mafunzo kwa sababu tunawalezi kinamama na kinababa kwenye makambi ambao wanawalea katika maadili mazuri,"alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Brigedia Jenerali Mabena kwa niaba ya Mkuu wa JKT, aliwataka wazazi na walezi wa vijana ambao wameanza kuripoti katika kambi hizo kutokuwa na wasiwasi wowote kwa sababu jeshi hilo linawafundisha vijana nidhamu na uzalendo kwa ajili ya kwenda kujenga taifa lao.

"Tunaomba wazazi msiwe na wasiwasi wowote juu ya malezi yanayotolewa na JKT kwa sababu tunafundisha vijana stadi za kazi na uzalendo unaowafanya wawe na nidhamu popote watakapokuwa,"alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Alifafanua zaidi ya kuwa mlezi yeyote atakayebainika anafanya vitendo vya kiunyanyasaji na ukatili wa kijinsia atachukuliwa hatua kali za kisheria .

Hivyo, aliwataka wazazi kuwaruhusu watoto kuendelea kujiunga na mafunzo hayo kwa mujibu wa sheria katika kambi ambazo zimeainishwa pamoja na vifaa ambavyo wametakiwa kwenda navyo.

Akizungumzia kuhusu maandalizi ya wanafunzi waliohitimu kidato cha sita kujiunga kwenye kambi, Brigedia Jenerali Mabena alisema tayari baadhi yao wameanza kuripoti kwa ajili ya kuanza mafunzo.

Alisisitiza zaidi ya kuwa wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu unaoonekana wanatakiwa kuripoti kwenye Kambi ya Ruvu JKT iliyoko mkoani Pwani.

## TCDC kuanzisha mfumo kuwabana viongozi matapeli

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imepanga kuja na mfumo wa kidijitali utakaosaidia kuweka uwazi kwenye vyama vya ushirika ili kukomesha viongozi ambao wamekuwa wakiendesha shughuli zao kitapeli.

Mrajisi na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dk. Benson Ndiege, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho Siku ya Ushirika Duniani itakayo fanyika kitaifa mkoani Tabora kuanzia Juni 26 hadi Julai 1, mwaka huu.

Alisema katika maadhimisho hayo mwaka huu Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Dk. Ndiege alisema hivi sasa wanapanga kuweka mifumo ya Tekonilojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo itasaidia kuongeza uwazi katika uendeshaji wa vyama vya ushirika nchini na kusaidia kuondoa ubabaishaji ulopo.

"Mfumo huu ukifungwa utawezesha hata mimi nikiwa hapa ofisi naweza kuona ushirika wowote na kutoa maelekeo kabla ushirika ule haujakufa,"alisema.

Alisema lengo ni kuwakutanisha wadau wa ushirika wakiwemo viongozi wa ushirika, wadau na viongozi wa serikali wanaosimamia sekta ya ushirika.

"Pia kutangaza kazi za wanaushirika, kuhabarisha umma juu ya falsafa na manufaa ya ushirika na kutoa fursa ya kujadili matatizo ya kiuchumi na kijamii zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi. kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni "Ushirika kwa maendeleo endelevu,"alisema Dk. Ndiege

Aidha, alisema maadhimisho hayo yataambatana na shughuli mbalimbali ikiwemo makongamano, utoaji wa zawadi, uchangiaji damu, upimaji wa afya, shindano la insha, burudani na michezo.

Pia, alisema maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani hutoa fursa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara kutoa huduma kwa washiriki hali inayosababisha ukuzaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja, uchumi wa mkoa husika.

Vile vile, alisema maadhimisho hayo husaidia kuwaunganisha wanaushirika na wabia wa maendeleo toka ndani na nje ya nchi na kuviunganisha vyama vya ushirika ili kuimarisha mahusiano katika kusaidiana masuala ya kiuchumi na kijamii.

Aliisema maadhimisho hayo pia husaidia washiriki kupata fursa za kielimu na kubadilishana uzoefu kupitia makongamano mbalimbali.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania, (TFC) Charles Jishuli, alisema ushirika umekuwa na tija kubwa nchini licha kuwepo kwa mitizamo hasi kwa baadhi ya watu.

# MAISHA

JUNI 4, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## JILAMBE NA MIHOGO YA KUKAANGA

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Tumia pazia kupendezesha nyumba yako




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# LIPSTICK INAPAKWA HIVI..

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | ■ | U | M | B | W | A |
| H | ■ | ■ | ■ | W | ■ | K |
| A | ■ | D | U | A | ■ | W |
| K | A | A | ■ | T | I | A |
| A | ■ | K | O | O | ■ | T |
| N | ■ | W | ■ | ■ | ■ | U |
| I | N | A | M | A | ■ | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


ZII, BEI, MJI, BUU, UMIMI, ZUBAA, AMANI, SAUTI, TAMBUKA, INGIZWA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

TAFUTA NJIA KUTOKA **A** KWENDA KWENYE BOKSI LA ZAWADI




## WATOTO

# PAKA RANGI




CHEKA

KICHEKESHO

Mhindi akijibu methali kwa kiswahili:
(a)Nyani haoni.....valisa miwani!
(B)Debe tupu....weka dengu!
(c)Masikini akipata....iko acha iba!
(d)Penye kuku wengi...chinja bili, tatu!
(e)Asiyesikia la mkuu....peleka yeye polisi!
(f)Penye wengi......iko kutano ya Chadema!

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Usiogope majaribu, udhia jitie nguvu tu utashinda

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze pale tulipoishia wiki iliyopita. Nazungumza na wale waliokata tamaa wakidhani kuwa hapo walipofikia kimaisha ndio mwisho. Hapana. Kuna kujitia nguvu, kisha usonge mbele kwani mafanikio yapo mbele yako.

Nikataja baadhi ya maana ya kujitia nguvu kwamba, ni kuvaa ujasiri wa kufanya jambo ulilokusudia kulifanya. Kuwa na moyo wa uhodari na ushujaa, kulinda kile ulichokiamini na kukisimamia bila hofu. Pia kuwa na tumaini kuwa haijalishi ni mazingira gani unapitia lazima utimize kusudi lako.

Nilitaja pia baadhi ya sababu kwa nini unapaswa kujitia nguvu nikasema; Mungu anakupenda na amewekeza vitu vingi ndani yako akiamini kuwa utafanikiwa.

Kingine nikasema yapo mambo mengine yanakutegemea wewe kufanya na siyo mtu mwingine. Upo wakati hupaswi kumtegemea mtu mwingine, usimame wewe mwenyewe!

Vile vile nikasema kama hutajitia nguvu mwenyewe utaibiwa. Kipengele hiki watu wengi hukipuuzia hivyo kujikuta wakiyumba kimaisha. Wanavunjika moyo, wanajuta, kukandamizwa na kutawaliwa na hofu. Unapojitia moyo, hupata nguvu ya kuvishinda vyote hivyo kwani ni viua hatma.

Msomaji wangu, leo nikuongezee vipengele vingine vitatu muhimu katika maisha. Ili ndoto zako zitimie, lazima ujitie nguvu. Upo wakati utatamani kuona ndoto zako zikitimia.

Isitoshe, kuna wakati utatamani kupanda juu zaidi ya matarajio ya adui zako! Upo wakati utatamani maono yako yatimie na kwa sababu hiyo, itakulazimu ujitie nguvu mwenyewe.

Mtu pia anapaswa kujitia nguvu ili asipoteze fursa kwenye maisha. Kuna wakati itakulazimu ujitie nguvu ili usipoteze ndoa yako. Au upo wakati itakubidi ujitie nguvu ili usipoteze fursa ya kazi au biashara ya ndoto yako.

Sababu nyingine ya kujitia nguvu ni kwamba unategemewa na watu wengine. Vile vile kwa sababu mke, mume wako, watoto, wazazi wako, ndugu na jamaa zako wanakutegemea.

Wakati kuna matatizo kwenye ndoa yako, utapaswa kujitia nguvu ya kuendelea kusimama ili watoto wako wasiathirike kutokana na matatizo yenu.

Jambo lingine nikuongezee hapa msomaji wangu ni kwamba, tambua udhia ni sehemu ya maisha! Unaweza kuuliza neno udhia lina maana gani?

Zipo maana nyingi, lakini hapa nikutajie chache. Udhia ni majaribu, mateso, misiba, huzuni, changamoto, kuumizwa na pia kujeruhiwa.

Unapoishi hapa duniani, udhia lazima utakupitia kama sehemu ya maisha. Siku zote kumbuka msemo huu kwamba, "umesamehewa dhambi, lakini siyo majaribu".

Udhia upo kwa mtu yoyote kama sehemu ya maisha haijalishi una cheo gani, upako gani(kwa watumishi wa Mungu), huwezi kukwepa udhia. Tena mwenye upako mkubwa sana ndipo udhia nao unakuwa mkubwa. Siku zote upako mkubwa unavuta majaribu na maadui wengi!

Kwa mantiki hiyo, hata kama unapitia mateso gani katika maisha yako hupaswi kukata tamaa. Maisha hayana tambarare, ni miinuko na mabonde lakini mwisho ni mafanikio makubwa.

Mwanadamu yeyote aliyekamilika lazima tu akutane na udhia katika safari yake ya maisha hapa duniani. Yapo majaribu mengi watu wanapitia katika maisha yao ya kila siku.

Majaribu haya yanatofautiana kulingana na mazingira mtu anaishi. Yupo mwenye jaribu katika ndoa yake. Rafiki yako wa karibu anatafuta kubomoa ndoa yako. Anatumia ukaribu wenu kuleta mtikisiko ili mradi tu aone maisha yanakuwa machungu.

Zipo silaha nyingi maadui hutumia kusababisha migogoro kwenye familia. Mfano maneno. Maneno ni nguvu, yakiachiliwa na kusambaa yanaleta madhara makubwa sana ikiwemo kwenye ndoa. Maneno ni sumu. Upo msemo kwamba heri mchawi kuliko mtu mwongo!

Jaribu lingine ni pale rafiki yako uliyemuamini anapokugeuka. Si unajua ule msemo kwamba adui yako ni wa nyumbani mwako? Yaani yule aliye karibu kabisa na wewe aweza kukujeruhi hadi ushangae. Si anakujua? Tuwe makini katika hili.

Majaribu yakikujia usiogope, usikate tamaa. Usiikimbie hali unayopitia, ikabili kwa kujitia nguvu kwa ujasiri kutimiza kusudi lako. Na Mungu anapoona hatua hiyo, huingilia kati kukusaidia na kukuokoa!

Wakati wa shida ni lazima tumtegemee Mungu. Wakati wa majaribu lazima umkaribie Mungu kwani peke yako huwezi. Moja ya neno lake linasema, "Mtumaini Mungu kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe".

***Msomaji wangu, bila shaka umejifunza jambo hapa. Tutaendelea wiki ijayo. Una simulizi ya kimaisha? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Utouh umenena, tunu za taifa ziimbwe na HEET!

DHANA ya uzalendo, uadilifu na uwajibikaji ni tunu ya taifa. Tunu za taifa ni mambo muhimu ya kujivunia kwa jamii yoyote ile kwa sababu tunu ndio msingi wa maadili na utamaduni wa jamii.

Mfano mzuri ni utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi na uwajibikaji. Kwa ni nini mambo haya yasiingizwe pia kwenye katiba mpya inayopendekezwa ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia mchakato wake kuanza?

Nakumbuka hata katika ibara ya tano ya rasimu ya katiba iliyoandikwa chini ya uongozi wa Jaji Joseph Warioba, iliainisha kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaenzi na kuzingatia tunu za taifa ambazo ni utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uwajibikaji na lugha ya taifa. Ikumbukwe kuwa katiba ya sasa haina tunu za taifa.

Hivi karibuni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Mstaafu (CAG), Ludovick Utouh, aliwaeleza wanazuoni nchini namna anavyoliona ombwe linalotishia uhai wa taifa kwa sasa kuhusu kupungua kwa uadilifu, uzalendo na kukosekana kwa uwajibikaji wa Watanzania. Hakuishia hapo tu bali aliwashauri wasomi wa vyuo vikuu kubuni na kutafakari njia sahihi za jinsi ya kushughulikia tatizo hilo.

Utouh, ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, alieleza ombwe hilo wakati akizungumza na wasomi mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), alipoalikwa kuzindua kamati ya ushauri wa uhusiano na sekta binafsi/soko la ajira, iliyopewa jukumu la kushauri katika mradi wa kitaifa wa elimu ya juu wa mageuzi ya kiuchumi (HEET).

Katika hotuba yake, Utouh aliitaka kamati iliyopewa kazi hiyo, isisahau jukumu moja muhimu la kubuni na kutafakari njia sahihi za vyuo vyetu vikuu nchini, kikiwamo MoCU kutafuta jinsi ya kushughulikia tatizo linalotishia uhai wa taifa la uhuishaji wa uadilifu, uzalendo na ukosekanaji wa uwajibikaji wa Watanzania.

Namnukuu: "Tunaweza tukafundisha watu wakawa na huo ujuzi, lakini kusema kweli bila ya kuwepo na uadilifu, kukawepo na uzalendo na watu wakaelewa kuhusu uwajibikaji, bado wahitimu wetu watabaki kujifunza. Uadilifu, uzalendo na uwajibikaji ni muhimu na una maana pana kwa taifa, kwa sababu ni muhimu sana kwa soko la ajira."

Aidha, Utouh alisema mradi wa kitaifa wa elimu ya juu wa mageuzi ya kiuchumi (HEET), mabadiliko makubwa ya mitaala yatafanyika sambamba na uboreshwaji wa miundombinu ikiwamo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mradi huo wa HEET, unafadhiliwa na serikali ya Tanzania chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB). Dhima kuu ya mradi huo ni kuwa na elimu inayoendana na soko la ajira.

Alisema kwa maono yake, anaamini nafasi ya ubora wa elimu ya juu, itaamuliwa kwa kiwango chake cha matumizi ya TEHAMA, ikiwamo kubuni mitaala inayoakisi maendeleo.

Utouh alisema anaona mpaka sasa vyuo vyetu vingi vimeendelea kutumia njia za asili na za kizamani katika kutoa mafunzo yake, yaani mwalimu na wanafunzi lazima muonane katika chumba kimoja cha darasa.

Ndiyo maana anatamani kuona vyuo vikuu vyote vya Tanzania, vinapanua wigo huo juu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Haiwezekani tukaendelea kukumbatia mitaala iliyopitwa na wakati, mafunzo yaliyopitwa na wakati na njia za ufundishaji zilizopitwa na wakati.


Huko ni kuwaacha wanafunzi bila ya kuwa na ujuzi ya kukabiliana na tatizo la mabadiliko yanayotokea kwa haraka duniani. Ni kweli taifa lolote ambalo halifanyi maboresho katika mfumo wake wa elimu, linahatarisha kuachwa nyuma kimaendeleo.

Kongole kwa serikali kuendelea na mapito ya sera na mafunzo ya elimu ya ufundi stadi ya mwaka 2014, ili kuwapatia wahitimu katika fani zote maarifa na ujuzi sahihi utakaowawezesha kujiamini, kujiajiri au kuajirika katika mazingira ya utandawazi na kukidhi mahitaji ya soko.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# BIBI HARUSI ZINGATIA NGOZI YAKO








KUOLEWA ni moja ya ibada iliyodhihirishwa katika vitabu vitukufu vya dini tofauti. Na kila mwanamke anafurahi wakati anasubiri jambo hilo kwa hamu.

Kama wewe ni bibi harusi mtarajiwa na unataka utokee vizuri siku yako hiyo kubwa zingatia kutunza ngozi yako kwa kupunguza mawazo, kupumzika muda wa kutosha, kufanya mazoezi, kupata mafuta mazuri ya kulainisha ngozi na scrub.










# MITINDO

Na Mary Geofrey







## Usisite kutokelezea kisa ujauzito

WANAWAKE wajawazito hupitia wakati mfupi wa kuchagua mavazi ya kuwafaa na zaidi hupata shida kupata nguo ambazo hazionyeshi tumbo.

Jinsi ya kuvaa wakati wa ujauzito bila kupoteza mtindo ni jambo ambalo wanawake wengi hujiuliza wakati wanaanza kugundua mabadiliko ya mwili.

Miaka kadhaa iliyopita nguo za wanawake wajawazito zote zilikuwa sawa na ni ngumu kupata katika maduka ambayo hayakuwa maalum. Lakini siku hizi kampuni zote za mitindo zina sehemu ya mavazi ya wajawazito.

Lengo ni kila mwanamke yeyote apate nguo zinazofaa kwa ujauzito, bila kupoteza mtindo wa kisasa na mavazi yanayoendana na bei za kawaida.

Wakati wa ujauzito nguo muhimu za kuzingatiwa kuwa nazo ni makoti ya ofisi, skafu na mitandio ya kisasa unayoweza kuvalia na gauni yako.



## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# Lipstick inapakwa hivi..

LIPSTICK ni bidhaa ambayo wanawake wengi husahau kutumia katika mapambo yao lakini kwa kweli ni zana yenye nguvu sana ambayo itakusaidia kuwa na midomo bora.

Kwa mwanamke ambaye hajawahi kupaka lipstick leo utajifunza jambo zuri litakalokusaidia kukuweka kwenye nafasi ya urembo zaidi.

Kwa wale ambao wamezoea kupaka lipstick leo tutajifunza njia salama ya kupaka lipstick ikawe vizuri kwenye midomo na kuongeza mvuto.

Andaa midomo yako

Hatua ya kwanza ya lipstick kuwa na matokeo mazuri ni kuandaa midomo yako. Kwa hili itabidi uondoe ngozi iliyokufa ambayo hukusanyika kwenye midomo yako.

Kuna njia nyingi ambazo unaweza kutuliza midomo yako lakini rahisi na ya bei rahisi ni jifanye kusugua mwenyewe. Itabidi uchanganye tu asilimia 50 ya sukari na mafuta ya nazi na kusugua midomo yako na kisha suuza vizuri. Itakuwa milaini sana.


Babies ndani ya mdomo

Tumia lipstick kupaka midomo yako ukimaliza chukua penseli ya lipstick uanze kuichora kufuata mwisho wa lips zako.

Wengi wetu tunapaka lipstick lakini tunasahau kutumia penseli kumalizia kupaka midogo yako ili kuweka msawazo mzuri.

Kwa kuongezea, ni muhimu kwamba unapotengeneza midomo yako usiende nje ya mstari wa midomo yako mwenyewe.





## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Jilambe na mihogo ya kukaanga

MSIMU wa mihogo umeanza kupamba moto na sasa ikipikwa inaiva vizuri.

Mihogo inaweza kupikwa kwa namna tofauti ikiwamo ile ya futari inayoungwa na nazi, inayochemshwa kwa kuwekwa maji na chumvi na ile ya kukaanga ambayo leo tutaelezea.

Mahitaji

Mihogo mikubwa mitatu, mafuta lita moja, kitunguu kimoja, kitunguu swaumu kiasi, tangawizi kiasi, nyanya nne, limao moja na karoti nusu.

Mahitaji mengine ni pilipili hoho nusu, pilipili manga kidogo, chumvi na pilipili mbichi.

Jinsi ya kupika

Menya mihogo, ikatekate kiasi upendacho na kwa urahisi wa kuiva kisha ioshe.

Bandika karai, tia mafuta, yakipata moto weka mihogo ukaange, angalia moto usiwe mkali sana ili mihogo iive polepoe bila kubabuka

Ikishaiva itoe uitie kwenye chujio ijichuje mafuta. Anza kuandaa kachumbari ya kulia mihogo.

Osha nyanya, karoti, hoho, tangawizi, chukua sufuria uvisage uvitie, kisha katakata kitunguu tia, twanga pilipili uitie. Weka chumvi na pilipili manga.

Bandika jikoni uweke na maji nusu kikombe na unyunyuzie mafuta kiasi. Funika acha ichemke dakika 5.

Kamulia limau uache ichemke kidogo, epua kachumbari yetu yakulia mihogo tayari.

Sasa mihogo yetu twaweza kuila muda wowote, kwa chai, maji na hata juisi na hata ukipata samaki wakukaanga hunoga mno.







MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

## Tumia meza ya bufee kutenga chakula

Na Restuta James

SEHEMU ya kulia chakula ni moja ya eneo muhimu ndani ya nyumba yoyote na ndio maana mtu anapojenga nyumba anazingatia eneo hili.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Simon Alex, anaeleza kuwa mabadiliko makubwa yanayoendelea kwenye sekta nyingine yameigusa pia sekta ya nyumba na mazingira kwa ujumla, akizungumzia eneo la chakula.

Akizungumzia meza ya bufee, anasema chakula hakipaswi kuwekwa kwenye meza ya chakula watu wanapokaa na kula.

Badala yake, anasema meza ya bufee ndio inayopaswa kuwekwa chakula na inatakiwa iwekwe pembezoni mwa meza ya chakula ili iwe rahisi kwa mtu anapopakua chakula kufika mezani kula.

Anasema meza hiyo inapaswa kuwa ndefu kiasi na sharti iwe na kioo kikubwa ili mtu anayepakua chakula aweze 'kutupia' jicho kujitazama.

Meza hii inaweza kuwekwa mshumaa, ua na glasi nzuri za maji, juisi na matunda, ili mtu anayesubiria chakula aweze kujipooza na kinywaji au tunda alipendalo.

Kwa mujibu wa Simon, mbali ya kuweka chakula, meza ya bufee ni 'pambo' nzuri ndani ya nyumba kwani inaongeza unadhifu na 'kupunguza' vyombo kwenye meza ya kulia chakula.





# Tumia pazia kupendezesha nyumba yako

PAZIA ni moja ya mapambo yanayotumika sana katika kupendezesha ndani ya nyumba.

Kama ilivyozoeleka, mapazia yamekuwa yakitumika kupamba mlangoni na dirishani. Mbali na majumbani, pia hutumika sana kupamba katika sehemu za ofisi, hotelini na sehemu nyingine nyingi.

Kadri ukuaji wa sayansi na teknolojia unavyochukua nafasi yake, kadhalika maisha nayo yanabadilika au kuboreka zaidi.

Kwa ujumla, mapazia katika kipindi hiki cha kasi ya ukuaji wa sayansi na tekonolojia, yamekuwa yakitengenezwa katika aina au mitindo yenye mvuto tofauti, hivyo kutoa fursa kila mtu kuchagua aina inayomfaa hasa kwa kuzingatia mandhari iliyoko ndani ya nyumba yake.

Pamoja na hayo, uchaguzi wa rangi na aina ya kitambaa kwa wale wanaopendelea kushona, nalo ni jambo muhimu linalopaswa kuzingatiwa. Wakati wa kufanya hayo yote kuzingatia aina ya rangi zilizoko katika nyumba yako kuanzia ukutani na vitu vingine vilivyomo ndani.

Kwa sasa, pazia lina umuhimu mkubwa katika kupendezesha nyumba ndiyo maana kuna umuhimu zaidi kuzingatia kufanya uchaguzi mzuri wa pazia hizo.

> **"Kwa sasa, pazia lina umuhimu mkubwa katika kupendezesha nyumba ndiyo maana kuna umuhimu zaidi kuzingatia kufanya uchaguzi mzuri wa pazia hizo.**

Ni vyema kutambua kuwa ubaya wa nyumba yako utatokana na namna wewe mwenyewe unavyoitengeneza na hata mvuto wake pia utategemea namna unavyochagua wewe.

Kila kitu kinawezekana ukijipanga, inawezekana kabisa usitumie gharama kubwa katika kupata pazia zako nzuri unazozipenda kama utajipanga na kudhamiria kuwa nazo.

Naamini wako ambao wanaweza kutundika pazia zao ndani ya nyumba kwa kutumia kamba za kawaida na ikapendeza lakini nashauri kama inawezekana si vibaya kutumia fimbo maalum za kutundikia mapazia hayo.


Fimbo hizi hupatikana kwa wingi katika maduka ambayo yanauza pazia kwa hiyo ni vema wakati unanunua pazia zako ukatafuta na fimbo yake.

Tafuta fimbo ambayo rangi yake inaendana na rangi iliyopo kwenye nyumba pamoja na iliyopo kwenye pazia.

Epuka rangi zinazong'ara sana kwa sababu hazina utulivu, ni vema kuchagua rangi iliyopoa.

Zingatia kuweka mapazia yako katika fimbo laini ambazo hazikwaruzi ili zisiharibu mapazia yako wakati unavuta kuziweka sawa.

# KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
sisi kama sisi wengine 'MAFISI' WanaonaGere Haoooooo!
JUKWAANI
MKE WANGU SURA GANI HIYO UNANIWEKEA ? WANAKUSHINDA HATA WADANGAJI WAKIWA HUMU!
NA BADO HAPA NATESTI MITAMBO BADO ILE YENYEWE YA MBUZI
NIMEMPIGIA BOSI WAKO KANAMBIA KESHAKUINGIZIA MSHAHARA TOKA WIKI ILIYOPITA UMEUPELEKA WAPI?
NIMEMLIPA FIDIA FATUMA ULIYEMUUMIZA ULIPOTU-FUMANIA
WE' NENG'ENEKA UNIFELISHE FIGO NIISHI KAMA ZOMBI NDIO UTARURAHI
POMBE HUZIWEZI BADO UNAZIGANDA HUTAKI KUACHA KAMA UMELOGEZEWA!
SHIKA ADABU YAKO SITAKI MSAADA WA MASIMANGO MI'NAJIMUDU NSHUSHE
BAR
WEWE MWENYEWE NDIO UMEYATAKA NIONEKANE UKWENI KAMA NIMEWATUSI WAKWE ZANGU, WAMEJUAJE KAMA UJANIREKODI NA KUWASIKILIZISHA?
HAPO NINGEKUWA MIMI, HUYO MKE NINGEMTWANGA TALAKA 'THALASA' NA MIGUMI JUU!
WEWE HUNA HEKIMA HUJUI HUYU KAMA KAWATUKANA WAKWE ZAKE HANA ADABU?
ALIYEMREKODI MUMEWE NDIO HANA ADABU KAWATUKANA WAZAZI WAKE KWA KUWASIKILISHA
KONDA DAI NAULI YAKO
MIE NDIO MAANA NAHAKIKISHA SIMU ZOTE ZIKO MBALI NDIO NALIANZISHA
KWA HIYO UNAUNGA MKONO HOJA IMEPITA?
KWA AKILI YAKO DALADALA UNAONA KAMA UKUMBI WA BUNGE NA ABIRIA NDIO WABUNGE, BANGI BHANA!
'NSHATUKANWA TAYARI... SUKA PAKI PEMBENI ILI HUYU MPUUZI NIMUONYESHE KAMA MIMI NAVUTA AU NALIPULIZA
HILI NI JESHI LA WATU WAWILI LAKINI HAPA UNA-MUONA MMOJA TU! MUULIZE VAN'DAME
WA PILI NTAMUONAJE WAKATI USHAMNYWA UMEBAKIZA CHUPA TUPU
HUYU MZARAMO ACHUNGUZWE ATAKUWA NA VIELEMENTI VYA KICHAGA AU KIHAYA SIO KWA HARUSI HII
*KINYUNYIZO CHA LEO... ULIYEMPIGA KIBUTI KADAKWA NA WAJANJA HAJAANGUKA...

## HABARI KIMATAIFA



Muonekano wa treni iliyopata ajali huko India, ikielezwa kuwa ndiyo ajali mbaya zaidi ya treni kuwahi tokea nchini humo katika karne hii. **PICHA: REUTERS.**

# Ajali ya treni yauwa takribani watu 280

**ODISHA,** INDIA

WATU takribani 280 wamepoteza maisha na wengine 900 wamejeruhiwa baada ya treni mbili za abiria kugongana katika Jimbo la Odisha nchini India.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na serikali ya India ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia jana, na kwamba inaingia katika rekodi za ajali mbaya zaidi kuwahi kutokea nchini humo katika kipindi cha zaidi ya muongo mmoja.

Inaelezwa kuwa ajali hiyo ilihusisha treni ya shirika la 'Howrah Superfast Express' iliyokuwa ikitokea Bangalore kuelekea Hawrah, Bengal Magharibi na treni nyingine ni ya shirika la 'Coromandel Express' iliyokuwa ikitokea Kalkata kwenda Chennai.

Mtendaji Mkuu wa Jimbo la Odisha, Pradeep Jena alisema idadi ya waliofariki kutokana na ajali hiyo inatarajiwa kuongezeka. Alisema kuwa zaidi ya magari 200 ya kubebea wagonjwa yalikwenda katika eneo la ajali katika wilaya ya Balasore ya Odisha na madaktari zaida ya 100, ikiwa ni kuwaongezea nguvu wengine 80 ambao tayari walikuwepo awali katika eneo la tukio.

Pia alibainisha kwamba video zilizopatikana katika eneo la tukio zilionyesha waokoaji wakiwa katika jitihada zao za kuwasaka manusura katika baadhi ya mabehewa huku kukitapakaa vilio vya baadhi yao wakiomba msaada.

Shuhuda mmoja ambae alikuwepo katika eneo hilo amenukuliwa na Shirika la Habari la Uingereza Reuters,

akisema "Nilikuwa pale katika eneo la ajali, nimeweza kuona kutapakaa kwa damu, viungo vilivyovunjika na watu wanakufakatika mazingira hayo."

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mamlaka nchini India imekuwa ikitoa taarifa zenye kupishana kuhusu kiini cha ajali hiyo, na kwamba hadi wakati huu hakujawa na majawabu ya treni ipi iliacha reli yake na kuigonga nyingine, na hadi wakati huu haijatoa taarifa ya kina kuhusu chanzo cha ajali hiyo.

Mamlaka nchini humo ilisema operesheni ya utafutaji wa miili ya watu na uokoaji ilianzishwa, ikihusisha mamia ya wafanyakazi wa idara ya zima moto, maofisa wa polisi na mbwa wa kunusa, na timu za kikosi cha kitaifa cha kukabiliana na maafa.

Vile vile, ilielezwa kuwa muda mfupi baada ya ajali hiyo, mamia ya vijana walijipanga nje ya hospitali ya serikali Odisha kuchangia damu.

Kwa mujibu wa Shirika la Reli la India watu takribani milioni 13 wanasafiri kwa kutumia treni kila siku, lakini mtandao unaoendeshwa na serikali umekuwa ukikabiliwa na changamoto za kiusalama na miundombinu yake kuzeeka.

**DW**

# Upinzani Uganda wataka mageuzi sheria za uchaguzi

**KAMPALA,** UGANDA

VYAMA vya upinzani nchini Uganda vimetaka katiba ya nchi hiyo pamoja na sheria za uchaguzi vifanyiwe mageuzi kabla ya uchaguzi mkuu wa 2026.

Kwa mujibu wa wanasiasa wa upinzani, Uganda haiwezi kudai kutawaliwa kidemokrasia katika mazingira ya sasa ambayo katiba imefanyiwa mageuzi kwa ajili ya kuendeleza utawala wa

Rais Yoweri Museveni, ambaye ametawala nchi hiyo tangu mwaka 1986. Viongozi na wabunge wa vyama vya siasa vya upinzani wameshiriki mkutano wa siku tatu kujadili mapendekezo wanayotaka kuwasilisha bungeni ili kuboresha utawala wa kidemokrasia Uganda.

Wakiongozwa na Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi Wine na Dk. Kizza Besigye, wanasiasa wa upinzani wametoa angalizo kuwa pana haja ya dharura kuhakikisha kuwa katiba ya nchi pamoja na sheria za uchaguzi vinachunguzwa upya. Kyagulanyi ambaye ni rais wa chama cha (NUP) alisema utawala wa Rais Museveni umetupilia mbali mamlaka za taasisi

mbalimbali ambazo zingelinda haki za raia na pia kutelekeza majukumu yao bila ushawishi wa kisiasa.

**DW**

## DRC yasaini Itifaki ya mkataba na ICC KINSHASA, DRC

**KINSHASA,** DRC

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na mwendesha mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC) Karim Khan, wametia saini hati ya makubaliano ya kuimarisha ushirikiano wao katika mapambano dhidi ya kutoadhibiwa kwa uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu.

Inaelezwa kuwa Khan, alifanya ziara ya siku nne nchini DRC, na kwamba walitia saini hiyo Juni mosi alipokuwa jijini Kinshasa.

Aidha, ilielezwa kuwa hakukuwa na taarifa iliyotolewa kuhusu maudhui ya mkataba huo, tangazo kuhusu ziara hiyo, wala safu mpya ya uchunguzi iliyofunguliwa, na kwamba hali hiyo haimaanishi kuwa uchunguzi hautafanyika.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa ICC iliombwa na mamlaka ya Kinshasa kushughulikia kesi kuhusu uhalifu wa vuguvugu la waasi wa M23, katika hatua ambayo mwendesha mashitaka huyo hakuzungumza lolote.

Khan, alikumbusha kuwa DRC ilikuwa mojawapo ya faili kongwe zaidi za ICC iliyofunguliwa mwaka 2004 kwamba tayari kumekuwa na hatia katika faili ndogo ya Ituri pekee.

Pia ilielezwa kuwa mwendesha mashtaka huyo wa ICC hakutaja uhalifu wa hivi karibuni na hasa matukio ya Kishishe Novemba 2022, ambayo ripoti hiyo inajadiliwa, ambayo yalisababisha mashirika ya haki za binadamu kuomba uchunguzi wa kimataifa.

**RFI**

### MARUDIO YA MNADA WA HADHARA

**RAISSA COMPANY LIMITED** tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana ya mdaiwa sugu kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.Mnada utaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| BISWARO ZEBEDAYO MSASE | Nyumba- iliyopo Mloganzila- Kwembe - Dsm | 15/06/2023 |

**Masharti Mengine:**

Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena.

Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**RAISSA Company Ltd:**
**0652113262/ 0757433333**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 50/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ASHA BAKARI SELEMANI WA MSAMVU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA IDDI SAIDI NAMATA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 06 Mwezi 06 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 2 mwezi 06 mwaka 2023

HAKIMU

### KUPOTEA KWA PASSPORT



**MENSIA ELIKANA KIMAMBO** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 428877** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **05 October, 2021.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/189332/2023.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NICODEMUS EMMANUEL MWANGOSI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **TOYOTA RAUM OLD MODEL** yenye namba za usajili **T 911 BVC** .

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi:
**MOR/MOR/RB/186401/2023**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 58 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**JOSEPHINA ELIAS MKOBA**

**By 1. ROMAN THOMAS MKOBA**
**2. ....................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **T. KANIKI** day of **13.06.2023.**

Dated at MOROGORO this 02 day of 6.2023

..............................
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P. O Box 660, Morogoro

## MAKALA

# USITUPE NYOKA NA MTI WAKE



Na Magabilo Masambu

**Jambo la muhimu si lazima kuwa na cha kuwapa, inawezekana kweli hujawa na cha kuwapa kama fadhila, lakini ile tu kufikiria na kuumia juu yao ni jambo jema linaloonyesha ni jinsi gani unathamini mchango wao, ile kukaa na kusema bila fulani pengine nisingefika hapa, inakufanya utende mambo mema kwa wengine na kwamba kama wewe ulitendewa, hivyo ukafika hapo basi hayo ukiyatenda kwa wengine pia watafikia mafanikio yao.**

MAISHA ni sawa na barabara ndefu ambayo kwa vyovyote vile haiwezi kukosa kona, milima na mabonde. Ili uyafikie mafanikio lazima uvuke viunzi vyote hivyo. Kuna baadhi utavuka peke yako, baadhi utavushwa.

Uhakika nilio nao ni kwamba, hata wewe unayesoma makala hii, kuna mambo kila ukiyakumbuka kuhusu maisha yako ama utalia au yatakufanya ukumbuke ulikopitia mpaka ukafika hapo ulipo. Jambo jema tu tuliloumbwa nalo ni uwezo wa kuyasahau maumivu yote pale tunapopata kile tunachokihitaji.

Maisha ni watu na kila aliyezaliwa kutika ulimwengu huu, amezaliwa si kwa bahati mbaya, hivyo kuna jambo atakalolifanya kwa ajili ya wengine. Hii ina maana kwamba katika umri wako ulio nao kama hujawahi kufanya jambo kwa ajili ya mtu mwingine yeyote, basi uwapo wako hapa duniani hautakuwa na maana zaidi ya kujaza nafasi na kuongeza idadi ya watu duniani.

Miaka ya nyuma, ilikuwa kawaida sana watu wasio ndugu kuishi pamoja na kulelewa kama ndugu wa damu kwenye familia, walioleiwa walitambua thamani ya kulelewa, hivyo walichochea sana waleaji kuendelea kulea wengine.

Leo ukilea hata mtoto wa nduguyo, mtaishia kukosana na pengine kutoongea kabisa kwa sababu ya mtoto mwenyewe.

Lakini zamani waliozeshwa kwa mahari za nyumbani, walifanya kazi kama watoto wa nyumbani, wengine tuliozaliwa baada yao wakati tunakua, hatukujua kama si ndugu wa kuzaliwa tulifahamu hivyo mpaka wanazeeka.

Ukichunguza maisha yetu ya kiafrika na hasa ya kitanzania, tulio wengi tumepitia mikononi mwa watu ambao wengine ni ndugu zetu wa damu na wengine ni watu baki.

Unaweza ukawa umefanikiwa kimaisha lakini ni muhimu kila wakati kutafakari na kujiuliza juu ya watu waliogusa maisha yako, inawezekana wengine hawapo wametangulia mbele ya haki na hivyo kuacha maumivu makubwa sana moyoni mwako, maana pengine ulitamani urudishe fadhila zako kwao lakini hawapo tena.

Jambo la muhimu si lazima kuwa na cha kuwapa, inawezekana kweli hujawa na cha kuwapa kama fadhila, lakini ile tu kufikiria na kuumia juu yao ni jambo jema linaloonyesha ni jinsi gani unathamini mchango wao, ile kukaa na kusema bila fulani pengine nisingefika hapa, inakufanya utende mambo mema kwa wengine na kwamba kama wewe ulitendewa, hivyo ukafika hapo basi hayo ukiyatenda kwa wengine pia watafikia mafanikio yao.

Kushikwa mkono inaweza kuwa kwenye jambo lolote. Inaweza kuwa kwenye elimu, biashara, siasa, uongozi na mahali popote ni muhimu sana kukumbuka ulikotolewa.

Kuna watu hawakuwahi kufikiri watakuwa viongozi, pamoja na kwamba uongozi hutoka kwa Mwenyezi Mungu lakini maono hayo ili yatimie yanahitaji msaada wa binadamu.

Kuna watu walipopata kazi wakaziamini elimu zao na kwamba walikuwa na akili sana darasani bila kufahamu kwamba elimu hizo zina mchango mpaka wa wapishi wa shule waliokuwa wanawapikia chakula wakiwa bweni, walinzi waliokuwa wanahakikisha kwamba wako salama, walimu waliowafundisha na kadhalika.

Unapofikia kiwango cha kutotambua mchango wa yeyote katika mafanikio yako, utakuwa mwanzo wa kutokumbuka ulikotoka. Unaweza kufanikiwa sana lakini mafanikio hayo hayatakuwa na baraka na madhara yake huwa hayaonekani waziwazi na kwa haraka.

Pamoja na maisha kubadilika kiasi cha kutotosha kuwasaidia watu wengi zaidi kama zamani, jambo la kutokumbuka tulikotoka limewakatisha tamaa sana watu wengi wema ambao wangeliwasaidia wengine.

Kuna msemo unasema tenda wema uende zako, lakini binadamu yoyote ameumbwa na hulka ya unafsi hata ukimweleza kwamba natambua mchango wako katika maisha yangu, anafurahi. Tusiwahitaji tu watu tunapotaka msaada kutoka kwao bali wakati wowote ule.

Kwenye eneo la siasa, hali ni mbaya zaidi. Historia inaonyesha kwamba maadui wengi wa kisiasa mwanzo kabla ya uadui walikuwa marafiki waliosaidiana kwa hali na mali.

Baada ya mmoja kutangulia kuyakalia madaraka, anayebaki hugeuka kuwa adui ni kama wasemavyo watu kwamba palipo na uadui wema ulitangulia. Kwa nini muwe maadui wakati maisha huisha?

Yuko mhenga mmoja aliwahi kusema unapokuwa unapanda ngazi, salimia waliyoko chini kwa sababu utawahitaji wakati wa kushuka kwako.

Tukirudisha fadhila kwa wale waliyowahi kutusaidia tutawapa nguvu ya kusaidia Zaidi.

Lakini tukitupa nyoka na mti wake, siku nyingine tutakosa mti wa kumpigia nyoka mwingine akijitokeza. Matokeo yake atatung'ata kabla hatujamgonga kichwani.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Ajali mbaya Kivukoni, kisa cha wimbo 'dereva Kombo.'*



Na Adam Fungamwango

MASHABIKI wa muziki wa dansi, wanapoenda ukumbini kuburudika na bendi mbalimbali zinazopiga 'laivu' ni lazima wakutane na wimbo uitwao 'Dereva Kombo' ambao wengi wanaufahamu kama 'Ajali Haikingiki.'

Si huo tu, lakini kuna 'Georgina', 'Rangi ya Chungwa', 'Karubandika', 'Ngoma Iko Huku', 'Embe Dodo' na zingine nyingi. Huwezi kwenda bendi zinazopiga muziki 'laivu' usikie nyimbo hizi zinapigwa.

Leo tutajikita kwenye wimbo wa 'Dereva Kombo.'

Wimbo huu ulirekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1960 na mwanamuziki mzaliwa wa kijiji cha Mbwabayanyundo Wilaya ya Kilifi, Mombasa nchini Kenya, Fundi Konde.

Ni mmoja wa wanamuziki maarufu mno ambaye mwishoni mwa miaka ya 1990 alikuja nchini Tanzania na kujiunga na bendi ya Shikamoo Jazz.

Alizaliwa Agosti 24, 1924 na kufariki dunia Juni 29, 2000 akiwa mmoja wa wanamuziki anayetambuliwa kama baba wa muziki wa Kenya.

Mbali na 'Dereva Kombo' alitunga na kurekodi nyimbo zingine maarufu kama 'Embe Dodo', 'Tausi Ndege Wangu' ambao ulitumika kwenye tamthilia iliyojulikana kwa jina hilo la Tausi, ikiwa na wasanii kama Mjuba, Siti Binti Kasri na Rehema,'Majengo Siendi Tena', 'Gari la Punda', 'Mazoea', 'Jabali', 'Jambo Sigara', 'Chaupele Mpenzi' na zingine nyingi.

Konde alitunga wimbo wa 'Dereva Kombo' kutokana na tukio la kweli lililotokea eneo la Likoni, kwenye kivuko au feri huko Mbombasa.

Hata hivyo, kuna taarifa kuwa mashairi wa wimbo huo hakutunga peke yake, badala yake alisaidiana na wanamuziki wenzake, Timoth Mwanyae na Paul Mwachupa.

Pamoja na hayo, kwenye hakimiliki ya wimbo huo, inaonyesha kuwa mtunzi ni mwenyewe Konde.

Wimbo huo ulitungwa kutokana na kisa cha kusikitisha. Basi lililobeba maharusi pamoja, ndugu, jamaa na marafiki waliambatana nao kutoka Tanga alikokwenda kuona bwana harusi na kurudi naye nyumbani kwake,

Mombasa kushindwa kufunga breki ndani ya pantoni na kutumbukia kwenye Bahari ya Hindi, Pwani ya Mombasa na kupoteza maisha ya watu wote.

Hiyo ilikuwa kwenye miaka ya 1960, lakini kwa sasa tayari daraja limejengwa eneo hilo la Likoni na kuwa ahueni kwa wananchi na nchi zote mbili, Tanzania na Kenya.

Walioshuhudia akiwamo mzee Timoth mwenyewe, anasema basi hilo lilikiwa na watu kiasi cha 60 hivi, wakiwamo bwana na bibi harusi.

Liliingia kwenye kivuko, ambacho kinafanana na pantoni zile za feri ya Dar es Salaam kutoka Magogoni kwenda Kigamboni.

Cha ajabu ni kwamba baada ya kuingia, lilishindwa kusimama na kutokea upande mwingine kwenye maji ya bahati likatumbukia.

Ikawa mwisho wa bwana, bi harusi, abiria wote waliokuwamo pamoja na dereva na basi hilo aliyejulikana na jina la Kombo ambaye ni Mbongo.

Sababu ya ajali hiyo imeelezwa kuwa ni mambo ya kishirikina. Pale kijiweni au stendi,

Pangani mkoani Tanga, wanapochukua abiria huwa wanafanya zamu kama ilivyo kwenye vituo vya bodaboda, bajaj, teksi na daladala. Dereva mmoja ambaye ni Mtanzania ilikuwa zamu yake kupakia na bahati iliyoje likaja kundi la zaidi ya watu 60 na wanaharusi, ambalo lilikodi kwenda Mombasa.

Gari halikuwaka na wakati wanalitengeneza, dereva Kombo alichukua tenda ya abiria wale na kuondoka nao kwenda Mombasa, akimwacha mwenye zamu yake akihangaika kutengeneza gari lake.

Jamaa alisikitika sana na kumwapiza dereva Kombo kama amemfanyia hila, basi kisasi kitalipwa. Na kweli basi halikufika lililokuwa likienda badala yake likaishia majini.

Kisa hicho kilitikisa Tanga yote hadi Mombasa. Wengi walijulia kuwa yule jamaa dereva aliyenyang'anywa tenda yake ndiye aliyefanya mambo ya kishirikina kwa dereva Kombo na ikawa kama mtego wa panya kuingia waliomo na wasiokuwamo.

Mzee Konde na wenzake walichukua kisa hiki na kukitungia wimbo huo ambao ni maarufu hadi leo. Mashairi yake ni haya hapa.

"Kweli ajali haikingiki, asainipo Mola mwenyewe, kweli ajali haikingiki, asainipo Mola mwenyewe, ni chombo imara, chenye thamani, kilichopasishwa Uingerezani.

Kiliunguma Likoni, kikatiririka, wale pasenja wakafelea baharini, kiliunguma Likoni, kikatiririka, wale pasenja wakafelea baharini, naona hivyo kwa herini.

Na Tanga Pangani, kwenye waganga na misahafu imepangana.

Dereva Kombo ungama zako zimekwisha, hapa Mombasa jirani wazi kwa shirika, dereva Kombo ungama zako zimekwisha, kwetu Mombasa jirani wazi kwa shirika, naona hivyo kwa herini.

Watoka Mombasa kwenda Nairobi, huko njiani maji saliti, Wanairobi hawana habari, mko njiani toka Mombasa. Mara radio yasema na jina ni Rango kwamba ajali mbaya imetokea njiani, nao pasenja hawajulikani majina, nayo hesabu ni ya kubahatisha. Fuateni wosia wa wimbo huu kwa kujiepusha na hizi ajali."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-13

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




WAHUDHURIAJI wote walikaa kimya wakimsikiliza Massawe, mtu pekee aliyepewa nafasi ya kuongea kwenye hafla hiyo ukiacha mwenyewe Belo.

"Niliporudi kuna vitu nilikuta haviko sawa, kwa hiyo ilibidi mimi mwenyewe nianze kuhaha huku na huko ili kuweka mambo yarudi kama yalivyokuwa mwanzo. Na katika kuweka mambo hayo sawa, katika kulizauliza, ndipo kuna watu wakanikutanisha na huyu bwana, anaitwa Belo, Ni mtu mzuri, mcheshi, na mpambanaji ambaye kwa ushirikiano wangu mimi na yeye umetufikisha hapa tulipofika.

Kifupi kuna tatizo limejitokeza kwenye biashara yangu. Na sikulijua tatizo hili hadi liliporejea kutoka Moshi.

Na limeleta matatizo makubwa sana na sijui, lakini leo hii hapa nitaweka wazi nini kimetokea na hadi nikaamua kuwasaka wahusika na bahati nzuri nikaangukia kwa Belo ambaye alinipa mbinu hii ambayo tumeifanya kabla watu hawafajafahamu lolote na mpaka sasa nadhani imekwenda vizuri.

Basi 'bethdei' ya leo inakwenda kuliweka jambo hili sawa, ili kila mmoja ajue leo nini kilitokea na nini kilifanyika hadi kila kitu kikawa shaghalabaghala.

Kwanza kabisa niombe samahani kwa sababu chanzo cha yote nitakayoyasema ni mimi hapa."

Alinyanyua chupa ya maji ya Kilimanjaro na kumiminia funda kadhaa mdomoni, akairudisha mezani, huku kila mmoja akiwa na shauku na kutaka kujua nini kitaendelea kusemwa kwani inaonekana kama kuna jambo hivi.

"Mimi kazi yangu kubwa ni fundi simu. Nimeifanya kazi hii kwa muda wa miaka mitano sasa. Na katika maisha yangu sijawahi kukutana na kitu ambacho nimekutana nacho.

Nakumbuka siku moja ofisini kwangu wateja zaidi kama 15 walileta simu ofisini mwangu nilizohitaji matengenezo.

Kwa kawaida wateja wengine huwa wanatoa laini zao na kuondoka nazo na wengine hawatoi. Nilizitengeneza baadhi na kesho yake wakaja watatu kuzichua, na wengine wakaja siku zinazofuata. Baada ya hapo mimi nilikwenda Moshi kwa ajili ya msiba wa baba yangu mzazi nikiwa sijui chochote.

Niliporejea, siku mmoja baada nikafuatwa na dada mmoja ofisini, akinilalamikia kuwa nimembadilishia simu.

**"Niliporudi kuna vitu nilikuta haviko sawa, kwa hiyo ilibidi mimi mwenyewe nianze kuhaha huku na huko ili kuweka mambo yarudi kama yalivyokuwa mwanzo. Na katika kuweka mambo hayo sawa, katika kuulizauliza, ndipo kuna watu wakanikutanisha na huyu bwana, anaitwa Belo.....**

Nimempa ya mtu mwingine. Sikuamini, nikaanza kuangalia simu zilizopo, hakuna ambayo hata inayofanana na ya kwake.

Akaniambia aliileta kabla hajaenda Moshi, tena ilikuwa na laini ndani, alisahau kuitoa, akasema aligundua hilo siku ya pili tu, lakini kila akija anakuta ofisi imefungwa.

Kusema kweli nilimuuliza kama nimempa simu ya mtu mwingine kwa nini huyo mteja mwingine asifike pale naye kulalamika? Akanijibu yeye hawezi kujibu hilo, lakini simu aliyonayo ni ya mtu mwingine inayofanana sana kwa muonekano ya kwake, lakini aligundua hilo baada ya kuiwasha na kupigiwa simu na watu asiowafahamu, baadaye akagundua si simu yake na hata laini ya mtu mwingine kwa kuepuka usumbufu, akaizima na hakutaka kuiwasha tena."

Habari hiyo iliwashtua baadhi ya wahudhuriaji, hasa wanaofahamu ugomvi wa simu ambao umesababisha mtu na mkewe humo kwenye sherehe kutengana.

"Nikamwambia simu ibaki pale kwa ajili ya uchunguzi na pia kusubiri nani mwingine atayekuja kulalamika, kwa sababu kama simu zimebadilishwa basi ni lazima yupo mwingine ambaye amechukua simu ambayo si yake na kama zinafanana basi atakuja tu.

Kwa bahati nzuri nilikwenda kwenye mgahawa mmoja wa jirani na ofisini kwangu kupata chakula cha mchana, yule dada aliyekuwa anatuhudumia alikuwa anazungumza na mwenzake habari za mwanamke mmoja wa jirani kuachana na mumewe kwa sababu ya kupigiwa simu na hawara ya mume.

Akamtaja jina kuwa ni Husna, ndipo nilipokumbuka kuna mteja mmoja alishawahi kuleta simu anaitwa Husna na hata kwa sura namfahamu. Baada ya kufikiria sana nikakumbuka alileta simu inayofanana sana na yule dada aliyekuja kunilalamikia. Kwa haraka haraka nikahisi kitu. Nikahisi simu ya dada yule aliyekuja kunilalamikia nilimpa Husna na huenda ndiyo ikawa imemletea matatizo."

Ilikuwa ni habari ya kushangaza na kusisimua kwa wakati mmoja. Kulibaki kimya kiasi hata ukidondosha sindano unaweza kuisikia. Kila mmoja alitaka kuisikia habari hiyo ya kutatanisha.

"Sikulala usiku, asubuhi nikamfuata yule dada wa kwenye mgahawa anisimulie kisa alichokuwa anazungumza na mwenzake jana. Akaniambia Husna kwa sasa ametengana na mkewe, baada ya kutukanwa kwa njia ya simu na mwanamke aliyejitambulisha kuwa na hawara ya mumewe. Nikamuuliza nitampataje yeye au mumewe, kwa sababu simu alipigiwa mtu asiyekusudiwa, akaniambia yeye hana mazoea sana na mumewe, na hajui Husna kwao ni wapi, lakini binti huo ana mpenzi wake ambaye ni rafiki yake Belo.

Ndipo tulipofanya utaratibu na dada huyo anaitwa Sarafina kupitia mpenzi wake kumpata Belo.

Nilipokaa na Belo na kuzungumza naye, akaniambia mdogo wake alimhakikishia hana mpenzi yoyote kwa sasa na haelewi mkewe alipigiwa na nani, tukawa na uhakika Husna alipigiwa simu na mwanamke mwingine, aliyempigia mwanamke mwingine."

Dan Nusura machozi yamtoke, akaanza kuhisi kuwa huenda 'bethdei' ile ingawa ni ya ukweli, lakini pia ilitumika kulitatua suala lake. Na kwa jinsi Massawe alivyokuwa akilihadithia, huenda ingechukua miaka mitatu mpaka mitano kugundua kitu kama hicho.

Akaanza kuhisi kuwa kaka yake Belo na Massawe, kabla ya kuwaalika hapa watakuwa wamefanya kazi kubwa ya kujidhihirisha kuhusiana na hili.

"Kabla hatujafanya chochote, tukampata dada aliyekuja kulalamika ofisini kubadilishiwa simu.

Alikuja tena ofisini kufuatilia simu na laini yake, tukambana kama hajawahi kugombana na mwanamke yeyote ambaye anamtuhumu kumchukulia mumewe, akakubali kuwa mara kwa mara amekuwa akipigiwa simu za mzaha kejeli, matusi na kashfa na mwanamke mmoja ambaye wanafahamiana, na sababu ni hiyo hiyo mume.

Basi hakukuwa na mjadala tena. Lakini ili kuwaita wote wawili mke na mume kwenye usuluhishi ni lazima tutengeneze plani kwa sababu,

Husna hakutaka suluhu yoyote. Ni kweli 'bethdei' ipo, lakini pia ilikuwa ni plani aliyoipanga Belo kwa ajili ya kuwakutanisha, tena mbele za wanafamilia, jamaa na marafiki ili pia waweze kupata somo. Mialiko yote hii hadi kwenda kwa mke wa Dan haikuwa ya bahati mbaya, ilikuwa na makusudi maalum."

Sasa kila mtu alielewa tatizo lilikuwa ni nini. Lakini bado wengi walikuwa na maswali ya kujiuliza. Wanawake hao waliogombana hadi kusababisha jambo hilo ni kina nani? Na Ilikuwaje hadi kutukanwa asiyehusika, na kwa nini Husna hakugundua kama simu ile haikuwa ya kwake baada ya kukoga matusi?

"Nimezungumza sana, kwa bahati nzuri tumefanya kila kitu sisi. Tumemualika dada ambaye simu yake ilibadilishwa na kupewa Husna na ya Husna kupewa yeye. Atasimama mtamuona, na sikutaka kulitaja jina lake kabla, yeye mwenyewe atajitambulisha." Massawe baada ya kusimama na kuzungumza kwa muda mrefu, aliketi.

ITAENDELEA JUMAPILI


# NYUMBA YA KANYE WEST, KODI MIL 47 KWA MWEZI


RAPA wa Kimarekani Kanye West na mkewe mpya Bianca Censori, wamehama walipokuwa wanakaa na sasa wamehamia nyumba nyingine mpya ya kifahari, ambayo kodi yake kwa mwezi Sh. Milioni 47 kwa pesa za Kitanzania.

Kwa mujibu wa Radar Online, awali wanandoa hao walikuwa wamekodisha chumba kwenye hoteli huko Nobu Ryokan, lakini kwa sasa wamepata nyumba maeneo ya West Hollywood.

"Baada ya miezi kukaa katika Nobu Ryokan huko Malibu, hatimaye wamepata nyumba yao wenyewe, karibu na Makao Makuu yake mapya huko Melrose ni nyumba nzuri, " watu wa karibu wa wanandoa hao wameeleza.

Hata hivyo imeelezwa jumba lake za zamani na kifahari alilolinunu zamani linaendelea kukaa tupu na kutelekezwa.







## Conboi ampa Khaligraph Till i Die

MKALI na ngoma za hiphop nchini Conboi Cannabino ameibuka tena na ngoma yake aliyoitoa mwaka mmoja uliopita 'Till i Die', lakini hii ya sasa akimshirikisha rapa kutoka nchini Kenya, Khaligraph Jones.

Ngoma hiyo imefyatuliwa Mei 26 mwaka huu na imeanza kusumbua mashabiki wa muziki huo kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki.

Ikiwa na maboresho machache hasa ya sauti ya mkali hiyo wa Kenya, ngoma mpya imepewa jina lile lile, lakini inajulikana kama 'Til i Die Ramix.'

Mara ya kwanza mwana hip hop huyo aliitoa ngoma hiyo, Aprili 22 mwaka jana, lakini kwa sasa ameamua kuifanyia marudio, akimshirikisha msanii huyo kwa ajili ya kupanua soko la muziki Afrika Mashariki.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**GUNDOGAN AKARIBIA BARCA**
NAHODHA wa Manchester City, Ilkay Gundogan, yuko mbioni kujiunga na Barcelona mkataba wake utakapokamilika msimu huu wa joto, huku klabu hiyo ya LaLiga ikimshawishi kiungo huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 32 kwa ofa ya mkataba wa miaka mitatu. (***Sport***)

**KOVACIC ANUKIA CITY**
CHELSEA itadai ada ya takribani pauni milioni 35 kwa kiungo wao wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic, mwenye umri wa miaka 29, ambaye anaonekana kukaribia kuhamia Manchester City. (***90 Min***)

**RICE, ARSENAL KIMEELEWEKA**
ARSENAL imefikia makubaliano ya kibinafsi na kiungo wa West Ham, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 24. (***FootballTransfers***)

**BAYERN YAKOMAA NA RICE**
KLABU ya Bayern Munich haijakata tamaa ya kumsajili, Declan Rice, kutoka West Ham baada ya kukutana naye jijini London, huku mabingwa hao wa Ujerumani wakipanga kuandaa ofa rasmi. (***Sky Sport***)

**MOYES AKALIA KUTI KAVU**
KLABU ya West Ham huenda ikamfuta kazi kocha wao, David Moyes, ikiwa hawatashinda fainali ya Ligi ya Europa Conference dhidi ya Fiorentina katika fainali itakayochezwa Jumatano. (***Guardian***)

**MAGUIRE CHAMBO KWA MOUNT**
MANCHESTER United itamtoa mlinzi wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 30 kwa Chelsea kama sehemu ya mabadilishano na kiungo wa kati, Mason Mount (24). (***Mirror***)

**BAYERN, UNITED VITANI**
BAYERN Munich na Manchester United bado zinavutiwa na mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic (23), ambaye yuko tayari kuhama msimu huu ikiwa Massimiliano Allegri, ataendelea kuwa kocha wa Juventus kwa sababu ya uhusiano wao mbaya. (***Nicolo Schira***)

**ALLISTER NJIA NYEUPE**
LIVERPOOL imekubali kufikia kipengele cha kuachiliwa kwa, Alexis Mac Allister na watailipa Brighton ada ya pauni milioni 55 kwa kiungo huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 24. (***Football Insider***)

**UGARTE KUSAJILIWA CHELSEA**
CHELSEA inatazamia kumleta mchezaji wa kimataifa wa Ecuador, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21 kutoka Brighton na mchezaji wa kimataifa wa Uruguay, Manuel Ugarte (22), kutoka Sporting Lisbon ili kuboresha safu yao ya kiungo. (***Guardian***)

**BARCA YAJIPANGA NA MESSI**
BARCELONA inaamini Ligi Kuu Hispania, LaLiga itaidhinisha mipango yao ya kifedha hivi karibuni, ili kuwawezesha kuanza mchakato wa uhamisho, ambao utajumuisha kusajiliwa tena kwa mshambuliaji wa Argentina mwenye umri wa miaka 35 na gwiji wa klabu hiyo, Lionel Messi, kwa uhamisho wa bure kutoka Paris St-Germain. (***90 Min***)

**MADRID: BENZEMA HAONDOKI**
KARIM Benzema atakamilisha mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Real Madrid, licha ya tetesi mshambuliaji huyo wa zamani wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 35, yuko tayari kukubali ofa kubwa ya kuhamia Saudi Arabia msimu huu wa joto. (***Marca***)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RAMOS RASMI KUONDOKA PSG

### Beki huyo Mhispania asema ilikuwa ni 'miaka miwili maalumu' katika...

**PARIS,** Ufaransa

SERGIO Ramos ataondoka Paris Saint-Germain baada ya mchezo wao wa mwisho wa msimu uliochezwa jana, mchezaji na klabu hiyo imethibitisha.

**Mkataba wa Ramos unaota rajiwa kumalizika msimu huu wa joto na hautaonge zwa tena na hivyo kumfan ya apatikane kwa uhamisho wa bure.**

"Nimeaga na sasa nafuata hatua nyingine ya maisha yangu, kwaheri PSG," aliandika Ramos kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii.

"Sijui ni sehemu ngapi mtu anaweza kujisikia yuko nyumbani, lakini bila shaka PSG, mashabiki na Paris walikuwa wapo pamoja na mimi.

"Asante kwa miaka miwili maalum ambayo niliweza kucheza katika kila mashindano na kujitolea. Nitakabiliana na changamoto mpya, nitavaa rangi nyingine."

Naye Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa PSG, Nasser Al-Khelaifi katika taarifa yake alisema: "Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Sergio Ramos kwa miaka miwili ambayo amekaa nasi.

"Uongozi wa Sergio, ari ya timu na kiwango chake, pamoja na uzoefu wake katika kiwango cha juu, vinamfanya kuwa gwiji wa soka wa kweli, na ilikuwa heshima kuwa naye Paris. Kila mtu katika klabu anamtakia kila la heri."

Ramos mwenye umri wa miaka 37 alijiunga na PSG msimu wa joto wa 2021 baada ya kukaa kwa miaka 16 Real Madrid, ambapo alishinda mataji matano ya LaLiga na mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mshindi wa Kombe la Dunia 2010 akiwa na Hispania, mlinzi huyo alicheza mechi 57 na kushinda mataji ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, katika misimu yake yote miwili akiwa PSG, lakini klabu hiyo ilishindwa kufuzu hatua ya 16 bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kufuatia msimu mwingine wa kukatishwa tamaa kwenye mashindano ya Ulaya, PSG inatarajiwa kufanyiwa mabadiliko makubwa msimu huu.

Kocha wa PSG, Christophe Galtier, alithibitisha Alhamisi Lionel Messi pia ataondoka mkataba wake utakapomalizika msimu huu wa joto, wakati vyanzo vimeiambia ESPN Neymar naye yupo tayari kuondoka.

Ramos pia alitangaza kustaafu kuichezea timu ya taifa ya Hispania Februari baada ya kucheza mechi 180.

Mbali na Kombe la Dunia, alishinda Kombe la Ulaya katika fainali za mwaka 2008 na 2012.

PSG, ambao walitwaa ubingwa wa Ligue 1 wikendi iliyopita, jana walikamilisha msimu wakiwa nyumbani kwa kuwakaribisha Clermont Foot Jumamosi.

HABARI MICHEZO

# Mourinho ashtakiwa kumtusi mwamuzi

**ROME,** Italia

SHIRIKISHO la Soka Ulaya (UEFA), limelaani kunyanyaswa kwa mwamuzi wa fainali ya Ligi ya Europa, Anthony Taylor na familia yake na mashabiki wa AS Roma, huku kocha wa klabu hiyo ya Ligi Kuu Italia maarufu Serie A, Jose Mourinho, akishtakiwa kwa kutumia lugha ya matusi dhidi ya ofisa huyo wa mechi.

Taylor alianza kushtumiwa na kutishwa baada ya Roma kupoteza kwa changamoto ya penalti dhidi ya Sevilla katika fainali hiyo iliyochezwa Jumatano iliyopita.

Mechi ilikuwa tete huku Taylor akiwa ametoa kadi za njano 14, zikiwa ndio kadi nyingi zaidi kuwahi kutolewa katika mchezo wa Ligi ya Europa.

Siku moja baada ya mechi, video zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii zikimwonyesha mwamuzi huyo wa England Taylor na familia yake wakinyanyaswa na mashabiki wa Roma kwenye Uwanja wa Ndege wa Budapest.

Katika video hiyo, mashabiki wa Roma walionekana wakimtusi Taylor (44) na familia yake, ambao walilazimika kupewa ulinzi kwenye uwanja wa ndege.

"UEFA inalaani vikali tabia ya vurugu inayoelekezwa kwa mwamuzi wake Anthony Taylor na familia yake. Vitendo kama hivyo havikubaliki na vinadhoofisha roho ya uchezaji wa haki na heshima ambayo UEFA inasimamia," ilisema taarifa ya UEFA.

"UEFA inadumisha ushirikiano wa karibu na polisi wa ndani na usalama wa uwanja wa ndege kuanzia waamuzi kuwasili katika miji waandaji.

"Hata hivyo, tunajitahidi kila mara kuimarisha hatua za usalama kwa maafisa kwa uratibu na mamlaka. Tutatathmini matukio kwa makini na kujumuisha maarifa muhimu katika michakato yetu ya kupanga matukio ya siku zijazo."

Kama sehemu ya taratibu za kinidhamu baada ya fainali hiyo, shirikisho la soka barani Ulaya siku ya Ijumaa lilimshtaki Mourinho, ambaye alirekodiwa akiwatolea maneno ya kashfa maofisa nje ya uwanja wa Puskas Arena.



Kocha huyo raia wa Ureno alimkosoa mwamuzi katika maoni yake baada ya mchezo, akisema, "ulikuwa mchezo mkali, wa kiume na wa kusisimua na mwamuzi ambaye alionekana Mhispania. Ilikuwa njano, njano, njano wakati wote."

Mashabiki wa timu zote mbili pia wameshtakiwa kwa kufyatua fataki na kurusha vitu, huku mashabiki wa Roma wakidaiwa kufanya uharibifu pamoja na fujo.

Sevilla pia wameshtakiwa kwa kuvamiwa uwanjani na mashabiki wao, ambao walitoka mbio hadi uwanjani baada ya Gonzalo Montiel kufunga bao la ushindi.



# MADRID YATANGAZA KUMWANIA HAVERTZ

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid inamfukuzia mchezaji wa Chelsea na raia wa Ujerumani, Kai Havertz, katika dirisha hili kubwa majira ya joto ili kuhakikisha wanaimarisha kikosi chao katika safu ya ushambuliaji.

Real Madrid inahitaji mshambuliaji mwingine ili kuboresha timu hiyo katika safu ya ushambuliaji na Havertz ameingia kwenye orodha ya wababe hao wa soka nchini Hispania.

Klabu hiyo inafikiria kutuma ofa kwa Chelsea kwa ajili ya kumpata mchezaji huyo huku Chelsea ikiwa tayari kumwachia mshambuliaji huyo.

Chelsea imeweka bayana itamuuza jumla na suala la kutolewa kwa mkopo sio kipaumbele chao hivyo wako tayari kusikiliza ofa kwa klabu ambazo zitakua zinataka huduma ya mchezaji huyo.

Madrid wao watatuma ofa kwa Chelsea lakini inafahamika klabu hiyo haipo tayari kutoa dau kubwa kumnunua Havertz, kwa sababu mchezaji pekee ambaye wamepanga kumsajili kwa gharama kubwa ni kiungo wa kimataifa wa England, Jude Bellingham, anayekipiga Borussia Dortmund.

Taarifa za mshambuliaji, Karim Benzema kuondoka klabuni hapo na kutimkia Saudia Arabia zimeifanya klabu hiyo kuanza kutafuta straika mwingine haraka.

# Forest kumtema Jesse Lingard

**LONDON,** England

JESSE Lingard anaongoza orodha ya nyota sita waandamizi ambao hawataongezewa mikataba yao na Nottingham Forest.

Kiungo huyo wa zamani wa Manchester United aliwasili hapo kwenye Uwanja wa City Ground msimu uliopita wa joto na akafanywa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika klabu hiyo, lakini amekuwa na wakati mgumu ya kuanza kwenye kikosi cha Kocha, Steve Cooper.

Akiwa ameanza katika mechi 12 pekee na tano akitokea benchi kwenye Ligi Kuu England msimu uliomalizika, Lingard atakuwa mchezaji huru baada ya kumalizika kwa mkataba wake wa sasa baadaye mwezi huu.

Kuna hakika kutakuwa na ofa kwa mzaliwa wa Warrington, ambaye alicheza mechi 232 katika mashindano yote akiwa na Mashetani Wekundu na alipelekwa kwa mkopo West Ham katika kipindi cha pili cha msimu wa 2020-21.

Lyle Taylor, Jack Colback, Andre Ayew, Jordan Smith na Cafu wote wanaelekea kwenye mlango wa kutokea pamoja na mchezaji huyo wa kimataifa wa England aliyeichezea nchi hiyo mechi 32.

Mshambuliaji Chris Wood pia atashuhudia uhamisho wake wa mkopo wa Januari kutoka Newcastle ukifanywa kuwa wa kudumu.

Forest walikosolewa sana kwa sera ya uhamisho ambapo ilisajili wachezaji wapya 22 msimu uliopita wa joto, na wakafanikiwa kubaki Ligi Kuu kwa pointi nne.



# SERIKALI YATANGAZA KUIPIGA 'STOP' LIGI KUU YA ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

LIGI Kuu ya Zanzibar iliyokuwa imepangwa kumalizika jana imesimamishwa ili kutoa nafasi kwa rufaa iliyokatwa na Black Sailor FC inayopingwa kupokonywa pointi katika mechi yao dhidi ya KMKM ambayo haikumalizika, imefahamika.

Mechi ya Ligi Kuu Zanzibar kati ya Black Sailor dhidi ya KMKM ilivunjika kutokana na kitendo cha wachezaji wa Black Sailor kumpiga mwamuzi baada ya wapinzani wao kusawazisha bao dakika ya 83 na kufanya matokeo kuwa sare ya bao 1-1.

Bingwa wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na inadhaminiwa na PBZ ilitarajia kupata bingwa wake katika mechi hizo za funga pazia.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada Vuai, alisema wamepokea barua kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Michezo Zanzibar ikieleza imesimamishwa michezo mitano ya kufunga rasmi pazia la Ligi Kuu ya Visiwani hapo mpaka rufaa ya Black Sailor itakapofanyiwa kazi.

Vuai alisema Black Sailor inapinga uamuzi uliotolewa na Bodi ya Ligi pamoja na Kamati ya Rufaa na Usuluhishi ya ZFF ambayo iliipokonya pointi timu hiyo na kuwapata alama tatu KMKM.

"Kamati zote mbili hazikutakiwa kusikiliza shauri hilo na badala yake Kamati ya Nidhamu ndio ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na kutoa uamuzi kwa mujibu wa Katiba ya ZFF," ilisema sehemu ya barua ya msajili huyo.

Aliongeza bosi huyo wa michezo aliagiza Kamati ya Utendaji ya ZFF kukutana ili kujadili vizuri matukio yaliyojitokeza siku ya mchezo huo ili kupata mwafaka kwa kufuata katiba ya shirikisho hilo.

"Napenda niseme Kamati ya Utendaj ya ZFF itakutana kwa haraka kufanya kikao chake ili kujadili kadhia hii kama inavyoelekeza barua ya msajili," alisema Vuai.

Bodi ya Ligi ilitoa adhabu kwa Black Sailor kwa mujibu wa Kanuni ya Mashindano ya ZFF ya kuwapokonya alama tatu, kufungia wachezaji wao watatu waliofanya fujo pamoja na kuwapiga faini wachezaji wa Black Sailor waliobainika kufanya ambavyo si kwa nidhamu.

Kati ya mechi tano za ligi hiyo zilizosimamishwa, mbili ndio zilitarajia kutoabingwa mpya wa msimu huu ambayo ilikuwa ni kati ya KMKM dhidi ya Chipukizi na KVZ dhidi ya Dulla Boys.

Maafande wa KMKM na KVZ, ndio wanachuana katika mbio za kuwania taji hilo.

Mechi nyingine zilizobakia ni kati ya Black Sailor dhidi ya Kipanga, Taifa Jang'ombe vs Kundemba na Jamhuri dhidi ya JKU.



Mshambuliaji wa timu ya Bulls, Ben Mango, akimtoka beki wa Under Future Star katika mechi ya mashindano ya soka ya vijana ya Dar Youth Cup (U-13), iliyofanyika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Polisi Tanzania yaitisha Simba*

**Na Shufaa Lyimo**

IKIWA katika vita ya kujinusuru na kushuka daraja, timu ya Polisi Tanzania imesema imejipanga kuonyesha kiwango bora katika mechi yake ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Polisi Tanzania inahitaji ushindi katika mechi hiyo huku ikiziombea timu nyingine zilizoko mkiani kupoteza michezo yao iliyobakia.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema wanafahamu Simba hawana cha kupoteza katika mechi hiyo lakini wao mchezo huo ni muhimu kwa sababu bado hawajakata tamaa.

Munisi alisema wamewaandaa wachezaji wao kupambana katika mechi hiyo kwa sababu uwezo wa kuondoka na pointi tatu na kurejea katika 'ulingo wa mapambano' wanao.

"Sisi tumeshakufa lakini wenzetu Simba wao wako I.C.U, wangetufikiria, tunahitaji ushindi kuliko jambo lolote, hawawezi kujua siku nyingine tutawasaidia nini," alisema Munisi.

Aliongeza ushindani uliopo katika msimu huu umesaidia kuiboresha na kuipa thamani Ligi Kuu Tanzania Bara, ndio maana vita ya kuwania ubingwa ilikuwa ndefu huku hadi leo bado timu nyingine itakayoshuka daraja na zile zitakazocheza 'play off' hazijajulikana.

"Hatutashuka kinyonge, vijana wameahidi kujituma kama ambavyo wamefanya katika michezo iliyopita, tulifanya kila jitihada, tuliboresha kikosi chetu pamoja na benchi la ufundi tukiamini tujiondoa mkiani, haikuwa hivyo," Munisi aliongeza.

Baada ya mechi hiyo, Polisi Tanzania itabakia Dar es Salaam kuwasubiri Azam FC katika mechi ya kumaliza msimu itakayochezwa Juni 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex.

# Ihefu SC yatarajia makubwa 2023/2024

**Na Saada Akida**

BODI ya Ihefu SC imesema itakutana mapema baada ya msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika ili kujipanga upya kuelekea msimu mpya ambao wamedhamiria kusajili kikosi cha 'daraja la juu', imeelezwa.

Ihefu imekuwa na msimu mzuri tofauti na miaka ya nyuma ambapo dakika hizi za lala salama ilikuwa kwenye 'joto' la kupambana kujinusuru kushuka daraja.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Zagalo Chalamila, kikao cha bodi yao kitafanyika baada ya kocha mkuu kuwasilisha ripoti ya msimu huu wa 2022/2023 ambayo itatoa mwongozo kuelekea msimu mpya wa mwaka 2023/24.

Chalamila alisema wamedhamiria kusajili wachezaji watakaoongeza nguvu na kuifanya Ihefu iwe timu yenye ushindani na inayoogopewa na klabu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema mbali na kusubiri ripoti, mabosi wa klabu hiyo watakutana na benchi la ufundi kufanya tathimini ya timu yao ambayo iliondolewa katika hatua ya robo fainali kwenye mashindano ya Kombe la FA.

"Bado hatujapokea mapendekezo yoyote kwa sasa kwa sababu hatujakutana na walimu wetu, tunatarajia kufanya kikao maalumu baada ya mechi ya mwisho ya msimu, kuhusu wachezaji wanaotajwa kuondoka hilo pia tunaliona na kusikia katika mitandao.

Kuhusu Mbegu (Yahya) kutakiwa na Simba, hilo halijafika kwetu na kwa sababu mkataba wake unafikia ukingoni mwisho mwa msimu huu tutafahamu nini uamuzi wake, Wadada (Nicholas) naye anahusishwa na Singida Big Stars, pia tunasikia ila tutakapopokea ripoti ya kocha wetu na kuangalia je nyota hao anawahitaji, tutakaa nao mezani ili kuwabakiza," alisema Chalamila.

Aliongeza wanatarajia kuingia sokoni kufanya usajili 'mkubwa' na watawabakiza wachezaji ambao watakuwa kwenye mipango ya kocha kwa sababu wanataka kufanya vyema zaidi katika msimu ujao.

" Timu yetu inaendelea kufanya mazoezi kama kawaida, tunataka kuhakikisha tunamaliza ligi kwa heshima, tunazitaka alama sita kutoka katika michezo yote miwili iliyobakia ambayo tutacheza nyumbani," Chalamila alisema.

Ihefu FC iko katika nafasi ya tisa ikiwa na pointi 33 na Jumanne itawakaribisha Geita Gold FC huku ikifunga pazia la msimu kwa kuwavaa Kagera Sugar.